


MABWANA, SISI

TUNATAKA KUMWONA YESU

 Asanteni sana. Bwana awabariki.

² Habari za jioni. Na ni majaliwa kuwa hapa, usiku wa leo, humu Dawson Creek tena. Miaka kama tisa iliyopita, nilikuwa na fursa, nafasi nzuri sana hapo awali, nilikuwa hapa juu kwenye likizo ndogo na kuhubiri upande wa pili wa barabara hapa mahali fulani, limenishangaza sana, huu mji umepanuka sana tangu nilipokuwa hapa mara ya mwisho kwa Ndugu Hunter, nilimfanyia ibada.

³ Ndipo nikaamua kwamba kama Bwana angenipa likizo nyingine, mbona, nilikuwa naja huku tena, kwa hiyo nilitaka kumheshimu Bwana wetu na—na kufanya ushirika pamoja na ndugu na dada wa imani moja yenye thamani. Kwa hiyo nimejaliwa kwamba ningeweza kusimama kwa siku tatu usiku mahali hapa pazuri padogo panapoitwa Dawson Creek.

⁴ Nami nina furaha sana kwamba ninaweza kuripoti kwamba tulisimama siku tatu usiku kwenye, mji ulio jirani yenu, Grande Prairie, na Bwana wetu alitubariki sana kule, nasi tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo. Nasi tunaamini ya kwamba Yeye atafanya tu jambo lile lile hapa, kwa sababu Yeye ni Mungu yule yule tu *hapa* juu kama alivyo *kule* chini, na Yeye—Yeye ni Mungu tu kila mahali.

⁵ Kwa hiyo sasa, nilifikiri usiku wa leo, kwa kawaida ninapokuwa Marekani na miongoni mwa watu ninaowajua, mwajua, na nimekuwa na ibada kadhaa, kwa kawaida mimi huchukua somo fulani na kuzungumza kwa ki—kitambo kidogo, lakini, halafu basi, na mikutano mikubwa, mbona, kwa kawaida meneja ndiye anayezungumza nami natoka tu chumbani mwangu katika maombi na kuingia na kuzungumza kwa yapata dakika tano, kumi kisha kufanyiza mstari wa maombi.

⁶ Lakini nikiwazia usiku wa leo, na, tungeweza tu kuzungumziana kwa muda kidogo na tungefahamiana zaidi, halafu nafikiri ingekuwa bora zaidi kama tungefahamiana vizuri zaidi. Nasi tunajua ya kwamba sisi ni Wakristo na raia wenza wa Ufalme wa Mbinguni, halafu kwamba tuko hivyo na labda hatujawahi kukutana hapo kabla maishani, vema, ni vema kama tukifahamiana zaidi kidogo. Niliwazia katika kufanya hivyo, huenda ukawa ni wakati mzuri sana kwangu ku—kufahamiana nanyi kwa namna fulani kuitambulisha mikutano.

Ninaamini maikrofoni imezimika mahali fulani, mimi, sina hakika, lakini ni—nilisikia sauti yangu ikiacha kutoa mwangwi

kule juu, na sasa nimerudi tena.

⁷ Kwa hiyo niliwazia kwa namna fulani ningewapa muhtasari mdogo wa mkutano. Kwa kawaida tunapoingia mjini au taifa fulani (Bwana ameniruhusu kwenda, karibu kila taifa ulimwenguni, nikifanya mikutano, nasi, tunamshukuru sana kwa ajili ya nafasi hii.), pamoja na ukosefu wa elimu na kadhalika ambayo ingehitajika kufanya mhudumu, Yeye amenipa, kwa neema Yake, njia nyingine ya kuzungumza na watu Wake, hiyo ni kwa kuwajulisha Maandiko ya “Yesu Kristo yeye yule jana, leo na hata milele,” yule Bwana Yesu mkuu, aliyefufuka.

⁸ Na katika hili, kwa kuona maono, ambayo yamekuwa, kitu ambacho nimekuwa na majaliwa ya kuona kutoka kwa Mungu tangu utotoni. . . Hapana shaka ila wengi wenu hapa mmesoma vile vitabu, na kadhalika, vya ushuhuda wa maisha yangu, na labda mmekuwa katika baadhi ya ibada. Lakini maono hayamponyi mtu yeyote, *hakuna* anayeweza kumponya mwingine. Na sehemu kuu ya ibada zangu imewekewa msingi, bila shaka, juu ya wokovu. Uponyaji wa Kiungu ni jambo dogo, wala hakuna mtu awezaye kulifanya kubwa jambo dogo. Lakini yapata asilimia themanini na sita ya huduma ya Bwana wetu ilikuwa ni uponyaji wa Kiungu, alifanya hivyo kusudi apate kuvutia macho ya watu.

⁹ Kama rafiki yangu wa thamani, mmoja wa wale, mameneja wangu wa kwanza, naye alikuwa pamoja nami mpaka alipokuwa mzee sana asingeweza kwenda, nafikiri mojawapo ya makanisa yake liko hapa mjini, linaloitwa Mwingano wa Kimishenari wa Kikristo, Dk. F. F. Bosworth, alizoea kuniambia, akasema, “Ndugu Branham, uponyaji wa Kiungu ni chambo unachoweka kwenye ndoana. Kamwe humwonyeshi samaki ndoana, unamwonyesha chambo, yeye hunyakua chambo akanaswa na ndoana.” Kwa hiyo hiyo ndiyo njia, kwa namna fulani kama vile, uponyaji wa Kiungu unavyotumiwa. Sisi. . . Bwana hufanya jambo fulani kuonyesha ya kwamba Yeye yupo, na wakati ma—macho ya watu yanapovutiwa kuona Uwepo wa Mungu yeye Yule aliyewaumba na atawahukumu kwenye ile Hukumu, wako tayari basi kuja upande Wake. Kwa hiyo ninashukuru kwa ajili ya nafasi hiyo.

¹⁰ Katika kufanya jambo hili, mara nyingi makusanyiko ni—ni makubwa, nasi tunawapa kadi ya maombi wapate namba, kisha tunaita namba hizo jukwaani na kuomba pamoja nao.

¹¹ Sasa, sijawahi kumponya mtu yeyote maishani mwangu mwote, lakini nimemwona Bwana akiwaponya makumi ya maelfu, ya taarifa zilizoandikwa kutoka kwa madaktari na hospitali kuu, kama vile Mayo, na—nami nimemwona katika huduma yangu fupi ya miaka ishirini na minane kwa ajili Yake, pamoja na taarifa zilizoandikwa, akiwafufua watu wanne

waliokufa kufikia leo, ambao tayari walikuwa wamepita pazia la wakati na wakafufuliwa, ambapo tuna taarifa kutoka kwa madaktari, ambao—ambao waliwatangaza wamekufa, na kufufuka tena.

¹² Na mara nyingi walionekana katika maono, kama lile la huko Norwe, ama, ninaamini, Finland, miaka michache iliyopita. Lilionekana kwa ono miaka mitatu au minne kabla halijatukia, nilimwagiza kila mtu aliweke katika Biblia zao kote katika mataifa na kadhalika, ndipo wakati ilipotimia, wakaona basi kwamba ilikuwa ni kweli.

¹³ Ninaamini kabisa, kweli kwamba karama na miito havina majuto, ninaamini ya kwamba ni karama zinazotoka kwa Mungu. Pia ninaamini ya kwamba kila kanisa la mahali hapo linapaswa kuwa na karama tisa za kiroho zikitenda kazi ndani yake, kulingana na Wakorintho wa Kwanza mlango wa 12.

¹⁴ Sasa, sisi, katika njia yangu ya kufundisha... Mimi si mfuasi wa dhehebu lolote, wakati mmoja nilikuwa mshiriki na nikafanywa mhudumu katika kanisa la Kimishenari la Kibaptisti, kisha nikaachana na hilo, si kwa sababu kanisa hilo lilikuwa na shida yoyote, lakini ni kwa sababu kwamba ningeweza kusimama katikati ya watu, kwenye pengo, na kuwa ndugu kwa watu wote, halafu ushawishi mdogo niliokuwa nao, ningeweza kuutoa kutoka kwa Bwana, haungeliendea shirika moja fulani, bali uwe kwa ajili ya makanisa yote na watu wote, na hilo lilikuwa ni chaguo langu la kufanya hivyo.

¹⁵ Ni majaliwa makuu, usiku wa leo, kuwa katika kanisa hili, shirika hili hapa ambalo—ambalo linamiliki kanisa hili, ambalo ninafahamu ni Kanisa la United. Siamini nimewahi kupata fursa ya kuzungumza kutoka kwenye mimbara ya—ya Kanisa la United hapo awali, nami ninayahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu.

¹⁶ Ninatumaini ya kwamba Mungu ataibariki halmashauri hii ya wadhamini iliyotupatia jengo hili zuri kwa ajili ya kumwabudu Mungu. Bwana na awabariki hao ndugu, ambariki mchungaji. Jalia likue kuwa kanisa lenye nguvu, nguvu sana, zaidi ya liliyvo sasa, kama hilo litawezekana, na kila kanisa ambalo limewakilisha hapa.

¹⁷ Tunawakilisha Kitu kimoja tu, hicho ni Kristo. Nao... Nafikiri Yeye ndiye Kitu kikuu cha ibada yetu na kuwekwa wakfu kwetu. Watu fulani huenda njia moja, wengine huenda *nyingine*, kama vile wakati mmoja niliingia jengoni, kulikuwa na m—mhudumu wa Kimethodisti, Kasisi Arnie Clagg, nilikuwa mhudumu wa Kibaptisti wakati huo, Bw. Bohanon alikuwa ameketi pale, Charlie Bohanon, ambaye alikuwa ni Mmasoni Mkuu awali, alikuwa msimamizi wa kampuni niliyokuwa nikifanya kazi, Padre Halpin, kasisi wa Kiairishi akaingia, naye akasema, “Sasa, sote tufanye nini sasa? Sote tumeketi pamoja.”

¹⁸ Ndipo maskini huyo kasisi akatoa ta—tamshi ambalo daima limedumu nami vizuri sana, alichukua kipande cha karatasi na kuchora bloku ndogo na kuandika, “Los Angeles,” akasema. . . ndipo basi akachora mistari kadhaa ikishuka kuelekea Los Angeles. Akasema, “Sasa, huyu *hapa* Billy,” huyo alikuwa ni mimi, akasema, “anashuka kupitia ile tunayoweza kusema ni Reli ya Pennsylvania.” Kasema, “Huyu *hapa* Ndugu Clagg naye anashuka kupitia ile wanayoiita Reli ya Kusini.” Na zingine mbalimbali, reli zikipita. Kasema, “Zote zinaelekea Los Angeles, kaa tu kwenye garimoshi lako.” Kwa hiyo nikawazia kwenye wa—wakati kama huo, hilo lilikuwa ni tamshi zuri sana kwa kasisi Mwairishi.

¹⁹ Na kwa hiyo huo ni, ukweli mwingi sana kwa hilo hata hivyo, ni kwamba jambo muhimu si *kile* unachoamini bali ni *Yule* unayemwamini, hilo ndilo. Nasi tunaamini, usiku wa leo, ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, aliyezaliwa na bikira Mariamu, akateswa chini ya Pilato, akasulubiwa, akafufuka siku ya tatu, kisha akapaa juu Mbinguni, naye ameketi kwenye mkono wa kuume wa Ukuu wa Mungu usiku wa leo, huko akiishi daima apate kutuombea tunapokiri. Kwa hiyo, Yeye asingeweza kutuombea mpaka kwanza tukiri kwamba Yeye ameifanya hiyo kazi, ni kazi iliyomalizika.

²⁰ Sasa, huenda nikatoa tamshi hili, ya kwamba uponyaji wote, wokovu wote ni—ni yale Mungu amefanikisha kwa ajili yetu kupitia Kristo, tayari ni kazi iliyomalizika. Sasa, kumbukeni hilo mnapoombewa, ama mwaambie marafiki zenu, kwamba hakuna kitu tunachoweza kufanya kuiboresha, hakuna kitu tunachoweza kufanya kuiendeleza, jambo pekee tunaloweza kufanya ni kuifundisha, mnaona, kwamba tayari imefanikishwa.

²¹ Mungu, Mwenyewe, alitufanyia hivyo pale Kalvari, na hapo, Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa; ni wakati uliopita. Sasa ni juu yenu na yangu kujitwalia imani, ndani yetu, kukubali yale Kristo ametufanyia, na mara tunapoikubali na kukiri kwamba Yeye amefanya hivyo, basi Yeye ameketi mkono wa kuume wa Mungu kufanya maombezi tunapoungama.

²² Sasa, neno *kuungama* hapo katika . . . ni neno lile lile, wahudumu hapa wangelijua, *kukiri* linasema, lakini *kukiri* na *kuungama* ni neno lile lile. *Kuungama*, lilikuwa “limeshaungamwa.” Linatokana na neno lile lile la Kiyunani.

²³ Nasi tunajua ya kwamba ni . . . hatuna budi kuungama ya kwamba Yeye amefanya jambo hilo, wala hawezi kulifanya mpaka tutakapoliungama, ndipo basi Yeye ni Kuhani Mkuu kufanya upatanisho juu ya yale tunayoungama kwamba Yeye ametufanyia, hiyo inafanya imani katika kazi iliyomalizika

ambayo Kristo alitufanyia pale Kalvari. Rahisi tu hivyo. Sasa, hiyo ni Injili isiyoghoshiwa.

²⁴ Sasa, leo hii unapozungumza juu ya uponyaji wa Kiungu, kidogo ni jambo nyeti miongoni mwa mengi ya makanisa. Ambapo mimi . . . katika ninii yetu . . . Marekani, na wengi wenu Wapresbiteri mnajua, kuna utafiti mkubwa juu ya, na—na magazeti kote nchini, na kadhalika, kwamba hatuna budi kurudi, kanisa la Kipresbiteri, kwenye mafundisho ya mwanzoni ya kimitume ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, kunena kwa lugha zingine, kufanya ibada za uponyaji, na kadhalika, mikutanoni.

²⁵ Mengi ya makanisa makuu Marekani yanajaribu kurudi kwenye mpangilio huo. Yule Billy Graham mashuhuri, katika tamshi lake hivi majuzi, katika hotuba moja, alisema, “Hatuwezi kupuuza kanisa la Kipentekoste tena,” kasema, “kwa sababu hilo ni moja ya makanisa makubwa yanayopanuka.”

²⁶ Ambalo kanisa la Kipentekoste linapanuka haraka sana kuliko makanisa yote yakiwekwa pamoja, madhehebu ya Kipentekoste. *Mgeni Wetu Wa Jumapili*, lile gazeti la Katoliki, mwaka jana lilisema kwamba kanisa Katoliki ulimwenguni kote walitangaza waongofu milioni moja jana usi- . . . , uh, mwaka jana. Lakini kanisa la Kipentekoste liliwaandikisha waongofu milioni moja na laki tano mwaka jana lenyewe, kwa hiyo linayashinda makanisa yote, kwa sababu ya shirika lake la kiinjalisti kote ulimwenguni. Na, bila shaka, hao ni wahudumu ambao wa—wanajulikana sana, ba—basi ni wangapi wa hao wengine ambao hatujui lolote kuwahusu?

²⁷ Sasa, lakini Pentekoste si dhe—dhehebu, Pentekoste ni tukio linalomwendea mwaminio yeyote. *Pentekoste* haiwezi kuundiwa dhehebu, Pentekoste ni tukio.

²⁸ Linaliendea kanisa la Anglikana, na kwa kanisa la United na kwa Methodisti, na Baptisti, na Wapresbiteri, “Atakaye na aje.” Ni kurudishwa kwenye ujumbe wa kimitume, ambapo kanisa Katoliki lenyewe lilianza wakati mmoja.

²⁹ Kanisa Katoliki, kanisa Katoliki la mwanzoni lilikuwa ni kanisa la Kipentekoste. Halafu basi, bila shaka lilijiundia dhehebu lake katika miaka mia tatu baada ya . . . kwenye—kwenye Baraza la Nikea, likaunda kile wanachokiita kanisa kuu la Kikristo la ulimwenguni kote.

³⁰ Na kutoka hapo ndipo akaja Martin Luther, na John Wesley, na loo, na kadhalika, kushuka chini, mpaka tuna madhehebu mia tisa na kitu mbalimbali sasa, bali msingi wa Ukristo wote ni Pentekoste. Na kama hilo lilikuwa ndilo wazo la Mungu la Kanisa kwanza, Mungu hawezi kukosea wala hawezi kubadilika, ndilo wazo Lake la Kanisa siku hizi.

³¹ Na huo ni ujuzi ambao mtu yeyote anaweza kuwa nao ambao ni wa yoyote ya madhehebu hayo, anaweza kuwa na ujuzi ule ule

katika madhehebu aliyomo, jambo muhimu ni kuupokea tu huo ujuzi.

³² Sasa, zaidi tungetaka kusema, ya kwamba kila usiku hao wavulana hushuka, na mwanangu hasa, nao wanawapa watu kadi ya maombi. Anazichukua hizo kadi za maombi, na kusimama mbele zenu, na kuzichanganya zote, yeye humpa mtu yeyote kadi ya maombi anayetaka moja.

³³ Sasa, jaribuni kuwa hapa kesho usiku kabla ya saa moja na nusu, kusudi tusikatize ibada. Usiku huo, ndipo tuje, hatuna njia ambayo tutaitia, hatujui mahali ambapo huenda ikawa, huenda tukaanzia moja hadi kumi na tano, ishirini, ama labda tuanzie ishirini, kinyumenyume, ama tuaanzie hamsini tuje *hivi, vile*, kuzichanganya tu pamoja kusudi watu wasije wakakusanyika na kusema, “Sasa, kama sina namba . . . kama sina tisini na tano hadi mia moja, nataka kuninii . . . Siitaki.” Mnaona? Lakini hujui mahali itakapoitiwa, tunangojea mpaka tutakapofika pale.

³⁴ Ndipo basi hilo linamfanya Roho aanze kutembea kwenye majengo, halafu huko nje kwenye kusanyiko, watu wanaanza kumwamini Mungu, naye Roho Mtakatifu anaingia moja kwa moja kwenye kusanyiko na kuchagua, inawatoa moja kwa moja kusanyikoni mle, popote walipo, kwa hiyo Roho Mtakatifu hafungiwi kwenye kadi ya maombi, ama kadhalika.

³⁵ Nayu kadi ya maombi ni namba tu ya kuzuia isiwe kama . . . Unasema . . . Ningesema usiku wa leo, labda watu mia mbili humu ndani, si—sininii . . . si mzuri sana kwa makadirio ya umati, lakini ningesema hatimaye, labda watu mia moja na hamsini, mia mbili. Vema basi kama ndivyo ilivyo, ningesema katika kundi hili dogo labda kungekuwa na watu hamsini waliotaka kuombewa.

³⁶ Hebu tuulize tu. Ni watu wangapi hapa ndani ambao, wana ugonjwa ambao mnetaka Mungu awaponye? Inueni mikono yenu, nyote, kila mahali. Mnaona? Zaidi ya nusu yao. Sasa, ni nani atakayekuwa wa kwanza jukwaani? Hapo—hapo ndipo una ninii . . . Hatuna budi kuwa na kadi ama njia fulani ya kufanya jambo hilo.

³⁷ Sasa, kesho asubuhi, nasikia, saa tatu kwenye Hoteli ya Windsor, kutakuwa na kiamshaki-. . . (nadhani tayari umetangaza hilo, sivyo, Ndugu?) Hilo ni sawa. Nami ninapaswa kuzungumza (Hiyo ni kweli?), kwenye kiamshakinywa. Nitafurahia mkija. Nafikiri ni kiamshakinywa cha watu wo—wote, tungefurahia mkija. Na—na—na halafu kesho jioni, tena, saa moja na nusu.

Sasa, na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja, tunapozungumza na Mwandishi wa hiki Kitabu tunachoenda kusoma.

³⁸ Mungu mwenye neema na Mwenye nguvu, Ambaye, kabla hata hakujakuwako na atomi hewani ama molekuli katika

atomi, Wewe ulikuwa Mungu. Na katika Kiumbe hiki kikuu kinachoitwa Mungu kulikuwa na sifa, kulikuwa na sifa kuwa Baba, sifa kuwa Mungu, sifa kuwa Mponyaji, sifa kuwa Mwokozi, wala hakukuwako na kitu cha kuokoa wala chochote cha kukuabudu Wewe, kwa hiyo Wewe ulikuwa tu Chanzo kikuu cha akili zote.

³⁹ Nawe ukawaumba Malaika, ndipo ukawa Mungu. Halafu basi kutoka hapo ukamwumba mwanadamu, na kadhalika. Mwanadamu akaanguka, nayo sifa kuu ya Mungu inajidhihirisha usiku wa leo, kama Mwokozi.

⁴⁰ Ulipomwumba mwanadamu ulifanyika Baba. Na sasa mwanadamu alipata magonjwa juu yake kutokana na kule kuanguka, kwa hiyo ile sifa kuu ya Mungu, ambayo ni kuwa Mponyaji, sasa inajionyesha yenyewe duniani kama Kristo Mponyaji.

⁴¹ Jinsi tulivyo na shukrani kwa ajili ya sifa hizi ambazo zimeonyeshwa katika maisha yetu wenyewe, ambapo tunajua ya kwamba tumepita kutoka mautini kuingia uzimani, kwa sababu jambo fulani limetukia ndani yetu ambalo limetutoa kwenye mambo ya ulimwengu hadi kwenye ushirika kama wana na binti pamoja na Mwenyezi Mungu aliye hai.

⁴² Mioyo yetu inafanywa kutetemeka kwa furaha kwa sababu ya tukio hili. Tuna furaha, Baba, na kujaribu kujihusisha na wengine, ili wengine waweze kufurahia baraka hizi kuu za ukombozi ambazo tumepewa kupitia mateso ya Bwana wetu.

⁴³ Wokovu wa nafsi, Roho Mtakatifu kutenda kazi miongoni mwa watu, na kuona uponyaji na miujiza ikifanywa, na mkono wa Mungu aliye hai ukitenda kazi miongoni mwetu, tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hili. Baba, ninaomba ya kwamba utawabariki ndugu na dada zetu kote katika Dawson Creek na maeneo yake kote, jalia kusiwe na mgonjwa au mtu anayeteseka miongoni mwetu ibada zitakapokwisha.

⁴⁴ Wabariki wahudumu wako, Bwana, jalia matokeo ya kukusanyika kwetu pamoja yaanzishe uamsho wa mtindo wa kale kote mko—mkoani, na ishara kuu na maajabu yaweze kuambatana na uamsho huu.

⁴⁵ Tunaamini ya kwamba tunaishi katika wakati wa mwisho, Baba, kama tulivyo katika mwisho wa siku hii, siku hii ya saa ishirini na nne. Tunaamini wakati jua linapotua kwenye... katika upeo wa magharibi, kwamba pia jua la ustaarabu linatua, na mwisho wa wakati umekaribia, nalo Jua la haki liko tayari kuchomoza likiwa na uponyaji katika mbawa Zake.

⁴⁶ Tujalie, Ee Bwana, ya kwamba haya yawe ni mambo muhimu sana kwa watu, wapate kufahamu kweli hizi ndogondogo na kuzishikilia, na wakumbuke kwamba siku moja kwamba kila mmoja wetu atapaswa kusimama katika Uwepo Wako adhimu na kutoa hesabu ya kila wazo linalopitia niani mwetu. Kwa

hiyo nipe mimi na watu wangu na watoto Wako juu ya nchi, mawazo safi, matakatifu, ya uaminifu, kusudi tusije tukajitenga na Maneno Yako, tukijua ya kwamba Neno Lako ni Kweli na Wewe ndiye Mungu asiye na kikomo, asiyeweza kukosea, aliyeko kila mahali, ajuaye yote, na mwenye nguvu zote. Basi, Baba, Wewe unajua mambo yote na Wewe upo kila mahali ku—kutufanyia mambo mengi mno kuliko yote tuwezayo kufanya au kuwaza. Nasi tunaamini ya kwamba Wewe utatujalia.

⁴⁷ Na Ee Baba Mungu, fanya jambo fulani hapa usiku wa leo, miongoni mwa watu ambalo litasababisha mshangao mkubwa sana katika mji huu mdogo. Tujalie, Baba, kwamba mioyo ya Mkristo itachochewa, na ifikapo Jumapili, jalia kila kanisa lijae pomoni, huku wenye dhambi wakitubu, ibada kuu za uponyaji zikiendelea kila mahali, ili kwamba kote nchini ipate kujulikana kwamba kuna uamsho wa Mungu aliye hai huko Dawson Creek, British Columbia.

⁴⁸ Baba Mungu, kwangu mimi, ninajilaza mwenyewe madhabahuni, itumie, Bwana, kwa njia yoyote unayoona inafaa. Sote tunafanya hivyo, na kuomba baraka Zako tunapoendelea kulingojea Neno Lako. Katika Jina la Yesu, tunaomba. Amina.

⁴⁹ Sasa, kwa njia tu ya—ya muktadha, ningetaka kusoma kutoka Yohana Mtakatifu 12:20 na 21, nichukue Andiko dogo linalojulikana kuzungumza tu, si kuhubiri, kwa sababu mimi—mimi, ninataka tu kuzungumza nanyi kwa njia ambayo, kuweka tu jambo hili kusudi mpate kuona, na hebu tuchukue dhana.

⁵⁰ Ninaamini Biblia ilisema, “Njoni, na tusemezane, asema Bwana,” katika—katika Isaya mlango wa 18. “Njoni, tusemezane, asema Bwana.” Sasa, nafikiri hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya, kusemezana.

⁵¹ Kwa hiyo katika njia tu ya, kusudi nipate muktadha, ninataka kusoma kifungu hiki:

Kulikuwa na Wayunani kadha wa kadha miongoni mwa watu waliokwea kwenda . . . sikukuu kuabudu:

Basi hao walimwendea . . . Filipo, mtu wa Bethsaida ya Galilaya, wakamwomba, wakisema, Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu.

⁵² Halafu katika Waebrania 13:8, tunasoma vifungu hivi hapa:

Yesu Kristo yeye yule jana, . . . leo, na hata milele.

⁵³ Sasa, hilo hapo swali kubwa. Na sasa, kugawa hili vizuri na kulitolea fa—fasiri ya busara, kadiri nijuavyo mimi ni hili: Kwamba sisi sote, tunajua kwamba kama Wakristo waaminio siku moja hatuna budi kusimama Mbele za Mungu. Tunajua hilo, hatuna budi kusimama Mbele Zake, kwa kuwa sisi ni viumbe vya uumbaji Wake.

⁵⁴ Na kama Wakristo, tunaamini ya kwamba Biblia hii ni Neno la Mungu lisiloweza kukosea. Mimi ni . . . Kama siwezi

kulikubali, kila Neno, basi si—siwezi kuwa na imani. Hu—huwezi kuwa na imani katika kitu ambacho—ambacho una shaka nacho, kwa sababu huna budi—huna budi kuwa na imani na kitu unachoamini.

⁵⁵ Kwa hiyo kama Neno linahitilafiana, ama lilikusudiwa kwa ajili ya wakati mwingine, ama watu wengine, na maandishi yaliyomo ndani Yake, baadhi ya Maandiko ni ya kweli na mengine si ya kweli, kama vile watu wangetufanya tuamini, ama kujaribu kutufanya, basi, kwangu mimi, Hiyo hata si. . . Ndi—Ndiyo kitu cha kutatanisha kuliko vyote, hata si—singekuwa Nacho nyumbani kwangu, kwa sababu siruhusu vitabu vya ulimwengu kuingizwa nyumbani kwangu. Na kama Kitabu hiki kinajipinga Chenyewe, ama kinaahidi kitu ambacho hakitaunga mkono, basi mimi. . . Si—Si Neno la Mungu.

⁵⁶ Sasa, kumbukeni, Mungu hana kikomo, Naye ni Mwenyezi. Naye yuko kila mahali, kwa sababu Yeye anajua yote, ama, na. . .

⁵⁷ Sasa, angalieni, basi Neno *hili* ni kweli, na kama ni kweli, ni Neno la Mungu; wala hakuna mtu aliye bora kuliko neno lake. Daima tunataka kusaini mikataba mmoja na mwenzake. Lakini kwangu mimi sikuzote ilionekana kana kwamba kama nikitia sahihi mkataba na mtu ambaye simwamini sana! Lakini kama nina imani na huyo mtu, hatutii sahihi mkataba wowote, neno letu ndilo linalosimama. Neno lako ndilo kifungo chako.

⁵⁸ Na kama siwezi kuwaambia ukweli, basi neno langu halifai chochote. Na kama Mungu ametwambia jambo ambalo si kweli, basi *Hili* si Neno la Mungu la sivyo Yeye asingeweza kuwa ni Mungu. Anawezaje kuwa ni Mungu asiye na kikomo, halafu aseme jambo lisilo kweli? Mnaona? Kwa hiyo ninaamini ya kwamba *Hili* ni Neno la Mungu, na kwamba mtazamo mzuri wa kiakili kuhusu yoyote ya ahadi hizo za Kiungu humo ndani utazifanya zitimie.

⁵⁹ Sasa, nawe- . . . Kuna . . . Ninasema kwamba huenda kukawa na ahadi humo ndani ambazo nisingeweza kuzifanya zitimie, kama vile Henoko alivyotembea na Mungu kwa muda wa miaka mia tano, kisha akafanya matembezi ya alasiri, akaenda Nyumbani pamoja Naye bila ya kufa. Laiti ningalikuwa na imani ya namna hiyo, bali nisingetaka kumzuia mtu mwingine aliyekuwa na imani ya namna hiyo. Kwa hiyo hatuna budi kuamini ni Neno la Mungu.

⁶⁰ Sasa, angalieni jambo hili, hao Wayunani walionyesha vizuri shauku ya kila mtu aliyepata kusikia habari za Yesu Kristo, kwa kuwa walisema katika ninii yao—yao. . . walichotaka ilikuwa ni, “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.” Hawakutamani kumsikia akifundisha, hawakuomba hata mojawapo ya miujiza hiyo waione, hawakusema, “Hebu nione ninii yako. . . miujiza ya

Yesu, hebu nimsikie akifundisha kwa muda kidogo.” Walisema, “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.”

⁶¹ Sasa, walikuwa na shauku, kwa sababu walikuwa *wamesikia* habari Zake. Sasa, “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno.” Sasa, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu.” Kwa hiyo walikuja kuona Neno lililofanyika mwili, Kristo alikuwa ni Neno la Mungu lililofanyika mwili.

⁶² Sasa, kama Yeye alikuwa hivyo wakati huo, akawaruhusu watu hawa kumwona Kristo, nasi, usiku wa leo, tungetamani kumwona, basi kwa nini tusingeweza kumwona vizuri tu kama walivyomwona? Sasa, ni wangapi humu ndani wangetaka kusema, “Mimi ningependa kumwona Yesu”? Hebu tuone mikonu yenu. Kote tu kwenye kusanyiko, haidhuru kama wewe ni Mkristo, mwenye dhambi, au la, “Ningependa kumwona Yesu.”

⁶³ Vema, kama hiyo ndiyo shauku yetu, na hiyo ndiyo shauku ile ile wale Wayunani waliyokuwa nayo waliokuja kwenye ile karamu. . . Ilikuwa ni sikukuu ya Pentekoste, na, walipokuja shauku yao, walikuwa wamesikia habari Zake, bali walitaka kumwona. Kwa hiyo walipata shauku yao kwa kuiomba kupitia mtumishi wa Kristo.

⁶⁴ Basi kama Yeye ni yule yule jana, leo na hata milele, basi hivi tusingeweza kupata shauku yetu jinsi walivyoweza, kama Yeye ni yule yule? Hivi si tunaweza kumwona kama tu walivyomwona? Kama siyo, basi Neno Lake lina kasoro, kwa kuwa Yeye alisema *hapa* ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Vema basi, kama tulikuwa tunaenda kumtafuta usiku wa leo. . .

⁶⁵ Na hebu ninukuu ahadi moja zaidi, ambapo sitajaribu kuchukua muda wenu mwingi kupita kiasi, maana ninajua khalima, na inawabidi kupanda mbegu zenu, na kadhalika, nami si—sitaki kuuchukua huo. Lakini tuna Mbegu hapa ambazo hukuza aina tofauti ya Uhai, kwa hiyo hebu tuchukue, tuweke Mbegu hizi mioyoni mwetu, kwa kuwa ni Uzima wa Milele kwa wote watakaolikubali na kuliamini.

⁶⁶ Sasa, Yesu alisema, “Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, nitakuwa hapo katikati.” Sasa, basi hilo halina budi kumleta mbele zetu sasa. Basi kama Yeye yuko hapa, Kristo asiyeonekana, basi kwa nini tusiweze kumwona kama wale Wayunani waliotaka kumwona? Kwa kuwa Yeye ni yule yule kwa kila njia isipokuwa mwili wa kawaida, mwili wa nyama, hasa, Yeye ni Kristo yeye yule.

⁶⁷ Vema, tungejuaje ya kwamba Yeye alikuwa hapa? Tungefahamuje ya kwamba Yeye alikuwa hapa? Sasa, Yeye alitoa ahadi za namna hii: “Bado kitambo kidogo, na ulimwengu

hautaniona tena, hata hivyo ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata ukamilifu wa dahari.”

⁶⁸ Sasa, Yeye aliahidi kuwa katika Kanisa Lake, akifanya kazi pamoja Nao, “Na kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya, nyingi kuliko hizi mtazifanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu.” Hiyo ni Yohana Mtakatifu, mlango wa 14, nafikiri kifungu cha 8. Kwamba tunaweza kufanya zaidi ya yale Yeye angeweza, ya King James inasema *kubwa zaidi*, lakini tafsiri ya asili ni *nyingi zaidi*, kwa sababu hakuna kitu kilicho kikubwa zaidi, Aliwaponya wagonjwa, akawafufua wafu, akasimamisha maumbile, bali ambapo Yeye alikuwa ndani ya Mtu mmoja, Mungu alikuwa wakati huo, sasa Yuko katika Kanisa Lake la ulimwenguni kote, kwa hiyo anaweza kufanya mengi zaidi kupitia Kanisa, kuliko angeweza kufanya katika Mtu mmoja.

⁶⁹ Sasa, tungetafuta mtu wa aina gani, kama tulikuwa tukitafuta huku Dawson, usiku wa leo, kumwona Yesu? Mngetaka kumwona, kwa hiyo tungemtafuta mtu wa aina gani? Je, tungemtafuta mtu aliyevalia mavazi yasiyo ya kawaida, mtu aliyevaa nguo za kidini, kama vile majoho au ukosi au kitu kingine cha kidini...? La, kwa maana Yesu alivaa nguo za kawaida. Yeye. . .

⁷⁰ Je, tungemtafuta mtu aliyeonekana tofauti na mtu mwingine? La, Yeye alikuwa ni Mwanadamu, alionekana tu kama mtu yeyote aonekanavyo, aliingia na kutoka, wanaume, hakuna mtu asiyejua ya kwamba Yeye alikuwa ni mtu wa kawaida tu. Na hapo ndipo Wayahudi wasingeweza kumfahamu Yeye kuwa, akijifanya Mwenyewe Mungu na hata hivyo akiwa ni Mwanadamu, kwa kuwa walimjua mama Ya—Yake na ndugu Zake na dada Zake, nao wakashangaa hekima hii yote kuu aliyokuwa nayo, ilitoka wapi.

⁷¹ Hakujua shule yoyote, Yeye, uh, kuhusu Yeye kuwa Mwe—Mwelimishaji, hatuna kumbukumbu ya Yeye kukaa hata siku moja katika shule yoyote mahali popote. Pia tuna kumbukumbu tu ya hata mitume, wote walikuwa, kwa jumla, watu wasio na elimu, wala maarifa. Yule aliyempendeza Kristo kumpa funguo za Ufalme, asingeweza hata kuandika jina lake mwenyewe.

⁷² Sijaribu kuunga mkono ujinga, ninajaribu tu kuwaambia, ya kwamba hatuwezi kuwaelimisha watu wamwone Mungu. Mungu hajulikani kwa elimu, wala sayansi, ama. . . Yeye anajulikana tu kwa imani, ndiyo njia pekee unayoweza kumpata, ni kwa kumwamini Yeye, huo ndio mpango alioweka, ili kwamba wasio na elimu na wenye elimu, pamoja, waweze kufurahia ushirika wa Uwepo Wake juu ya msingi wa imani katika Neno Lake.

⁷³ Kwa hiyo tungemtafuta mtu wa aina gani kama tusingemtafuta mtu wa aina hiyo? Tunaona jambo kama hilo siku hizi, silisemi kwa kukosoa, bali nalisema ili—ili niwe mkweli, ambapo tunaona makanisa yetu siku hizi yamevalia

majengo mazuri mno, tunaona huduma yetu katika mavazi mazuri sana, na—na kwaya zetu, na ninii yetu . . . pamoja na u—u—uimbaji ulio bora sana, tunaona wahudumu wetu wakiwa—wakiwa na Ph.D., L.L., digrii za kila namna, lakini yuko wapi huyo Yesu?

⁷⁴ Dk. Morris Reidhead, rais wa Misheni kuu za Sudan, zilizo kuu sana ulimwenguni, alinjia hivi majuzi, na mle chumbani, akasema, “Ndugu Branham, nina digrii nyingi, pamoja na digrii za heshima za kutosha kuukandika ukuta wako.” Akasema, “Lakini yuko wapi Kristo katika yoyote ya hayo? Kwani walimu wamekuwa makosani?”

⁷⁵ Nikasema, “Nisingependa kusema hivyo, Bwana.” Nikasema, “Mimi, kama m—mtu mwenye elimu ya shule ya msingi, nisingeweza kusema ya kwamba hao walimu mashuhuri, wazuri wamekosea, lakini, wamewaambia ukweli, lakini Kristo haendani na digrii ambazo mnazipata hapa kupitia theolojia, Kristo ni kwa imani, Yeye si hadithi ya kubuni, Yeye ni Mtu.”

⁷⁶ Roho Mtakatifu si wazo, ni Mtu, “Wakati Yeye, Roho Mtakatifu, atakapokuja,” na *yeye* ni kiwakilishi nafsi, kwa hiyo Hi—Hilo ni kweli kabisa, Ni Utu wa Kristo katika umbo la Roho Mtakatifu anayeishi ndani yako.

⁷⁷ Yesu alisema, “Mimi ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi.” Sasa, mzabibu hauzai matunda, matawi ndiyo yazaayo matunda, kwa hiyo basi, Yeye hana budi kututumia mimi na wewe, macho yetu, midomo yetu, kusikia kwe—kwetu, hotuba yetu, yote, huyo ni Yeye akinena kupitia kwetu, “Mimi ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi.”

⁷⁸ Kwa hiyo ingekuwa ushirikiano wa Kristo ndani ya watu Wake, kama tungeweza kumwona akitenda siku hizi kama alivyofanya wakati huo, kwa kuwa ni ahadi kwa Kanisa Lake, “Mkikaa ndani Yangu na Neno Langu ndani yenu, ombeni mtakalo.” Loo, maelfu mengi sana ya ahadi zingeweza kunukuliwa hapa. Lakini ni Kristo katika Kanisa Lake.

⁷⁹ Yale tuliyo fanya miongoni mwetu sote, nadhani niko kwenye kusanyiko lililochanganyikana, kama kawaida, lakini kile tulichofanya, tumemhusisha Kristo na wazo la kiakili la Mungu fulani wa kihistoria. Endapo Yeye ni Mungu wa kihistoria, atatufaa nini leo hii? Kama Yeye si Mungu yeye yule wa kizazi hiki kama alivyokuwa katika wakati wa mitume, Mungu wa Musa angefaa nini kama Yeye hakuwa Mungu yeye yule leo? Mungu wa uponyaji angefaa nini ambaye aliwaponya wagonjwa huko nyuma katika siku zake, na, iwapo Yeye si yeye yule leo?

⁸⁰ Kama ningepigia swali uponyaji, bila shaka ningetilika shaka wokovu, kwa sababu zote mbili ni arabuni za wokovu wetu . . . za kukamilishwa kwetu. Kama . . . Tunayo tu arabuni sasa ya ukombozi wetu mkamilifu.

⁸¹ Unapoweza kuona kivuli cha mtu mwenye kansa ya sarkoma, amegeuka akawa mtu mpya tena na kufanywa mzima na mwenye nguvu, hiyo ni ishara ya kwamba tutakuwa na mwili uliotukuzwa siku moja, kwa sababu ni Mungu aliye hai tu angeweza kufanya mwujiza kama huo.

⁸² Ninapoweza kumwona mwanamke mtaani aliye duni sana, aliyejishusha, mtovu wa uadilifu, ama mwanamume kutoka kwenye baa, akivuta sigara, na kunywa pombe, na kulaani, na kufanya yasiyofaa, na muda wa siku chache, yeye ni mtakatifu, mtu mtauwa, akiyalipia makosa yake yote, hiyo ni kusema, hiyo inaonyesha ya kwamba jambo fulani limempata mtu huyo. Mnaona? Inazungumza juu ya Nchi nyingine.

⁸³ Sisi ni raia, si wa Canada, sisi, wala sisi si raia wa Marekani, uraia wetu ni wa Juu. Sisi ni raia wa Ufalme wa Mungu.

⁸⁴ Ninapoenda Ujerumani, ninaangalia jinsi wafanyavyo, wana mawazo yao wenyewe. Nilishuka kutoka kwenye mmoja wa mikutano mikubwa sana, ambako tulikuwa na wastani wa watu elfu kumi waliookoka kila usiku, elfu hamsini wakaokoka katika muda wa siku tano usiku, halafu, hawa hapa hao watakatifu wameshika bilauri kubwa mno za bia, wakishuka kuja barabarani wakinywa upesi tu walivyoweza kunywa, wakimsifu Bwana sana walivyoweza. Mnaona? Vema, wao, hiyo ndiyo desturi yao huko Ujerumani, mnaona, hawalijali, na kadhalika.

⁸⁵ Mnaona tabia mbalimbali katika mataifa mbalimbali, tunazipata huku Canada, tunazipata Marekani. Lakini basi, Mkristo anapokuwa Mkristo, yeye si raia wa ulimwengu huu tena, kwa kuwa tunajua dhahiri ya kwamba sisi ni Uzao wa Ibrahimu, naye alikiri kwamba alikuwa msafiri na mgeni, alikuwa ni raia wa Ulimwengu mwingine, akiutafuta Mji ambao Mjenzi na Mbuni wake alikuwa ni Mungu.

⁸⁶ Kwa hiyo sisi, uraia wetu ni wa Juu, na Juu ni utakatifu, na usafi, na nguvu, ufunuo. Kwa hiyo, sisi ni raia wa Ufalme wa Mungu, na kama raia wa huo Ufalme, hebu na tumtazamie Mfalme wetu.

⁸⁷ Anaonekanaje? Tungempata wapi? Njia pekee ya busara ningeweza kukwambia, rafiki yangu, usiku wa leo, ni kurudi katika Maandiko na kuona kile alichokuwa jana, basi kile alichokuwa jana, atakuwa kitu hicho hicho leo na atakuwa milele, kwa sababu Yeye ni Mungu asiye na kikomo, asiyekosea, asiyebadilika.

⁸⁸ Na sasa, hebu turudi nyuma, hebu na tuweke kando, nitaweka kando mapokeo yangu ya Kibaptisti, wekeni kando Methodistu yenu, na mapokeo ya Kipentekoste, hebu turudi moja kwa moja kwenye Maandiko tuone Yeye alikuwa ni nani. Sasa, hilo linapaswa kuwa la kimantiki, la busara. Halafu basi, tutaona kama tunaweza kumwona au la, kama atatuzuru, usiku

wa leo, nami nina hakika tungefurahi sana kama Yeye angefanya hivyo.

⁸⁹ Angalieni, hebu turudi nyuma, tunasoma kutoka katika Yohana Mtakatifu mlango wa 12, hebu turudi kwenye mlango wa kwanza wa Yohana Mtakatifu na kuanza. Tunaona, mara baada ya kuzaliwa Kwake ya kwamba huduma Yake ya hadharani ilianza.

⁹⁰ Jambo la kwanza tunalomwona akifanya lilikuwa ni kuwaombea wagonjwa, Naye kwanza kabisa alihusishwa na uponyaji wa Kiungu, akiwaombea wagonjwa. Miujiza mikubwa iliambatana na maombi Yake, kwa kuwa Baba alikuwa akijibu maombi ya Mwanawe.

⁹¹ Ndipo tunajua ya kwamba kulikuwa na watu katika siku hiyo waliokuwa wakimtazamia Masihi. Hebu tusipoteze hoja hii sasa, walikuwa wakimtazamia Masihi, Aliyetiwa Mafuta, Kristo aliyekuwa ameahidiwa na manabii wa Agano la Kale. Kote tangu Mwanzo kuendelea, walikuwa wameahidiwa Masihi ajaye, kila kizazi kilimtazamia Masihi huyo ajaye.

⁹² Lakini jambo la kushangaza, wakati Yeye alipofika, walikuwa wamezama sana katika mambo mengine, hata wakashindwa kumtambua kuwa ni Masihi. Walikuwa wa kimtindo sana, wameshikana sana miongoni mwa... wakitengana wao kwa wao, Mafarisayo na Masadukayo na kadhalika, kama tu ilivyo siku hizi.

⁹³ Kwa hiyo ishara ile ile ambayo Masihi huyo alipaswa kuonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi aliyetumwa na Mungu, walikosa kuiona, kwa sababu ya uhusiano wao na ninii yao, ama, ushirikiano wao na dhehebu lao. Hebu niseme jambo hili kwa uchaji na upendano wa ndugu: karibu ni vivyo hivyo leo.

⁹⁴ Sasa, wakati Yohana Mbatizaji alipojitokeza jukwaani, huduma ya miujiza ilitokea kwenye jukwaa la mahubiri ya ajabu, kitu kama utaratibu wa Billy Graham, ambacho tungesema leo hii, wakati huduma hiyo kuu ilipokuja, watu walishangaa, na wengi wao walidhani moyoni mwao ya kwamba huyu alikuwa ndiye Masihi. Lakini akawaambia yeye hakuwa Masihi, alikuwa tu ni mtangulizi, kwamba Yeye angekuja nyuma yake. Ndipo wakati Yesu alipokuja, na, Yohana akamtambua kwa ishara, kwamba kule nyikani, Mungu Baba alikuwa amemwonyesha Yohana ya kwamba asingedanganyika katika kumwona Masihi wa kweli, kwa sababu angekuwa na ishara iliyomfuata.

⁹⁵ Sasa, hatuna budi kukumbuka ya kwamba Masihi, kulingana na mafundisho ya Agano la Kale, ali-...kulingana na Mwanzo, ama, Kumbukumbu la Torati 18:35, Yeye alikuwa awe Nabii. Musa, yule nabii mkuu wa Agano la Kale, aliyeweka dini ya Kiyahudi katika utaratibu, alisema ya kwamba

“Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii, kama nilivyo mimi. Itakuwa kwamba mtu yeyote asiyemsikia Nabii huyu atakatiliwa mbali na watu.” Na inaendelea na kuendelea kusomwa juu Yake.

⁹⁶ Mafundisho yote ya Agano la Kale yalielekeza kwa Masihi ajaye, na wahusika wote wa Agano la Kale walimwakilisha Masihi huyu mpaka lilipotimia katika Mtu. Daudi, akiulilia Yerusalemu, baada ya kukataliwa, mfalme aliyekataliwa, miaka mia nane kutoka hapo, Mwana wa Daudi aliketiki kwenye mlima ule ule, Mfalme aliyekataliwa na watu Wake Mwenyewe, na kuulilia Yerusalemu, “Yerusalemu, Yerusalemu!”

⁹⁷ Yusufu, mwana aliyezaliwa miongoni mwa ndugu wengine, huko kulikuwa kuzaliwa kwa njia ya kipekee, naye alizaliwa kuwa mwonaji, aliota ndoto, na kuona maono, na kadhalika, naye alichukiwa na ndugu zake kuonyesha mfano wa siku yenyewe tunayoishi sasa. Na huko ndugu zake walikuwa watu mashuhuri, wale wazee wetu, lakini hatimaye wakamwua, kama tu walivyomwua Kristo, akatupwa shimoni, akauzwa kwa karibu vipande thelathini vya fedha, akatwaliwa juu na katika kufungwa kwake, mmoja alipotea na mwingine akaokolewa na mchinja nyama na, ama, mwokaji na mnyweshaji. Na kwa hiyo katika kufungwa kwa Yesu msalabani, mmoja alipotea na mmoja akaokolewa.

⁹⁸ Ndipo baada ya yeye kuinuliwa kwenye cheo cha juu sana katika—katika ufalme, kwenye mkono wa kuume wa Farao, ambapo Yesu aliinuliwa kwenye wadhifa wa juu sana Mbinguni, mkono wa kuume wa Mungu. Ndipo Yusufu alipotoka akaenda, tarumbeta ililia, “Kila mmoja piga magoti yako, Yusufu yuaja.” Jambo lile lile wakati Baragumu itakapolia, “Kila goti litapigwa, na kila ulimi utamkiri Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.” Tunaona yote yakifananishwa.

⁹⁹ Mwangalieni Eliya, na kuendelea mbele, wote walikuwa ni mfano, hadi kwa Yohana. Na ndipo Masihi akatokea kulingana na hao watu huko nyuma waliotiwa mafuta na Roho Wake, Naye alikuwa Mungu kamili katika Umasihi, Yeye alikuwa ni Mungu aliyetiwa mafuta, Nabii.

¹⁰⁰ Na wakati alipokuja kufanya ishara hizo miongoni mwa watu, baadhi yao walikuwa wamezama *sana* katika imani ya kanisa lao, hata wakakosa kumwona Yeye. Sasa, hebu na tuyasimulie maisha Yake, hebu tumwone katika mlango wa kwanza wa Yohana Mtakatifu. Moja ya mambo ya kwanza tunayomwona akifanya: Kulikuwa na mtu jina lake Andrea, aliyekuwa amemwamini, akimshawishi ndugu yake, Simoni, aje amwone Mtu huyu.

¹⁰¹ Simoni, ambaye baadaye alikuja kuwa Petro na akapewa funguo za Ufalme, askofu mkuu wa Kanisa, mvuvi, asiye na elimu, Biblia ilisema, asiye na elimu, Mtakatifu, uh, Kitabu cha

Matendo mlango wa 3, kwamba alikuwa asiye na elimu wala maarifa, na kadhalika, na Yohana pia.

¹⁰² Na ndipo tunapomwona akitembea kuja Uweponi mwa Mtu huyu, Ambaye alidhaniwa kuwa ndiye Masihi, hebu tuangalie kile alichona. Vipi kama angalimwona mtu ambaye alikuwa tu ni mwanatheolojia mashuhuri? Walikuwa na wengi wao siku hizo. Mnaona? Walikuwa na wengi sana. Je, yeye...? Aliona nini? Si mwanatheolojia mashuhuri, lakini alimwona Jamaa mdogo, mnyenyekevu. Na mara alipoingia katika Uwepo Wake, alimtazama usoni na kusema, “Jina lako ni Simoni, na jina la baba yako ni Yona.” Na mara mtu huyu aliyefunzwa vizuri katika mambo ya kiroho akatambua ya kwamba Huyo alikuwa ndiye Masihi.

¹⁰³ Mamia ya miaka tangu walipokuwa na nabii, nao walijua aliyefuata alikuwa ni Masihi, sasa, kumbukeni hilo, mara moja, mtu huyu akatambua Huyo kuwa ndiye Masihi, naye akaanguka miguuni Pake.

¹⁰⁴ Kulikuwa na mtu aliyesimama pale jina lake Filippo, aliyeona hili likifanywa, na katika kuliona likitukia, akamkumbuka rafiki mwema. Kuna jambo fulani kulihusu, unapomwona, Kristo, kweli, huna budi kumwambia rafiki yako, mtu yeyote anajisikia hivyo kuhusu rafiki yake.

¹⁰⁵ Kwa hiyo anazunguka mlima, maili kumi na tano, naye anafikia mahali ambapo rafiki, ambaye alikuwa ni msomaji mashuhuri wa Biblia, na jina lake lilikuwa Nathanaeli, naye akampata chini ya m—mti, huko nje kwenye bustani ya mtini, akiomba, basi wakati Filippo alipomjia, alimwambia, baada ya maombi yake, “Njoo, umwone Yule tuliyempata!”

Sasa, kumbukeni, si Dk., Ph.D. Mnaona? Si mtu aliye na mwanatheolojia mashuhuri. “Tumemwona Masihi, aitwaye Kristo.”

Kasema, “Vema, Yeye ni Nani?”

Kasema, “Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusuifu.”

¹⁰⁶ Loo sasa, hilo kweli lililingusa mtu huyo, kwa sababu alikuwa amejihusisha kidogo—kidogo na kanisa, kwa sababu alikuwa mwothodoksi, naye akasema, “Sasa, laweza neno lolote jema kutoka Nazareti?”

¹⁰⁷ Kwa maneno mengine, “Ungeweza m—mji mdogo maskini kama huo, ama tabaka la watu maskini ambao umepotoka na—na—na kunenwa maovu, unaojulikana kote nchini mwetu kama mahali pabaya, wao ni wajinga, na ni wauaji, na maharamia, na kadhalika, laweza neno lolote jema kutoka Nazareti?”

¹⁰⁸ Na laiti kila mtu angechukua mtazamo huu, jambo lile lile ambalo...naye Nath...ambalo yeye, Filippo, alimwambia Nathanaeli, alisema, “Njoo, uone.” Haya basi, “Usikae nyumbani na kukosoa, njoo ujionee mwenyewe.”

¹⁰⁹ Njiani, laiti ningaliweza kuwasikia wakizungumza, hapana shaka ila kwamba walikuwa wakinena kuhusu kile Masihi alipaswa awe. Vema sasa, Nathanaeli alikuwa mtu mwenye elimu, vema, alisema, “Hapana shaka, hakika, ninajua kile—kile ishara ya Masihi itakuwa, kwa sababu Yeye atakuwa ni Nabii.”

Sasa, labda mazungumzo yao yalikuwa hivi: “Unamkumbuka yule mvuvi mzee, kule chini, jina la—lake Simoni?”

“Naam, ninamkumbuka.”

“Vema, unakumbuka hata asingeweza kutia sahihi jina lake kwenye risiti ya samaki wako.”

“Loo, hakika. Ninamjua yeye na baba yake, pia.”

¹¹⁰ “Alikwenda mbele ya Mtu huyu sasa, anayetoka Nazareti, huyu Nabii wa Galilaya, na mara alipokuja Mbele Zake, Yeye alimwambia jina lake lilikuwa ni Simoni na kwamba ali- . . . jina la baba yake lilikuwa Yona. Haitanishangaza ila kwamba Yeye angekwambia wewe ni nani.”

¹¹¹ Vema, ingekuwa ni vigumu kwa Filipino kuamini hilo. Lakini sasa, kumbukeni marafiki, ninasema nini? Ninajaribu kuwaambia nini? Hivyo ndivyo umma ulivyojua ya kwamba hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Yesu, Masihi.

¹¹² Sasa, ningetoa changamoto kwa hilo: Hakuna mtu anayeweza kupinga hilo, hiyo ni kweli, ilikuwa ni ishara ambayo ilipaswa kuwa pamoja na Masihi.

¹¹³ Vema, mara Filipino alipokuja Mbele Zake, na kumleta Nathanaeli, Yesu aligeuka na kumtazama, na kusema, “Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!”

¹¹⁴ Hilo lilimpunguzia majivuno mfuasi huyu wa kanisa. Hakujuu kabisa ni nini. . . Akasema, “Rabi,” (maana yake, “mwalimu,”) “ulinijua wapi Wewe? Hujawahi kuniona, hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana. Ungejuaje kwamba mambo kama hayo yalinihusu mimi?”

Akasema, “Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.” Huko kote kuzunguka mlima huo. Ni macho ya jinsi gani! Mnaona? “Nilikuona.”

¹¹⁵ Sikiliza nukuu hili. Ndipo ikawaje? Nathanaeli alianguka chini bila shaka, na kumtazama Yeye na kusema, “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ni Mfalme wa Israeli, yule Mtiwa Mafuta mkuu, kwa kuwa ninajua ya kwamba Maandiko yalitwambia ya kwamba hiyo ingekuwa ndiyo ishara ya Masihi. Hakika Wewe Ndiwe ambaye tumemtarajia.”

¹¹⁶ Vema, kama huyo alikuwa ni Yeye jana, akijitambulisha Mwenyewe kwa watu Wake, vema, Yeye ni yule yule leo, Maandiko yanasema ndivyo alivyo.

117 Loo, bila shaka sasa, kulikuwako na wale waliosimama pale ambao hawakuamini hilo, nao walikuwa waamini- . . . , uh, waorthodoksi hodari, wanasoma huku wamegeuza migongo yao, na majoho yao na kadhalika, wamevaa vilemba vyao vikubwa na kadhalika, pamoja na bendera yote ya kidini na mafundisho ya sharti ambayo wangeweza kuwa nayo.

118 Wakisimama pale wakiwa na vyeo vikuu vya majina yao na mambo kama hayo, na kusanyiko lao likiwepo, wakijua ya kwamba itawabidi kuwajibika kwa kusanyiko lao kwa ajili ya jambo hilo, wasingeweza kulipinga, hilo hapo, maajabu yalifanywa, ilibidi jambo fulani linukuliwe. Nao walisema nini? Wakasema, “Mtu huyu ni Beelzebuli, mkuu wa pepo, mpiga ramli, anasoma mawazo yao.”

119 Sasa, wakati wao. . . hawakusema kwa sauti kubwa, waliwazia moyoni mwao, Biblia ilisema, naye Yesu, akitambua mawazo yao, akageuka na kusema, “Nitawasamehe hilo, lakini siku moja Roho Mtakatifu yuaja, na atakapokuja Yeye atafanya jambo lile lile, na kunena neno moja dhidi Yake hakutasamehewa kamwe katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao.” Kwa hiyo mnaona mahali tunaposimama basi, katika siku hii.

120 “Baada ya kifo cha Yesu Kristo na kuikanyaga ile Damu ya Agano, tuliyotakaswa kwayo, na kuiita kitu kichafu, na kuzidharau kazi za neema, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi.” Waebrania mlango wa 6. Kwa hiyo mnaona mahali tulipo, tunazidharau kazi zenyewe za neema ambazo zimetuita kwenye utakaso, mnaona, kunena neno dhidi Yake.

121 Sasa—sasa, Yeye alikuja kwa nani? “Alikuja kwa walio Wake.” Walio Wake walikuwa ni nani? Waebrania, Wayahudi. Sasa, kulikuwako—kulikuwako na makundi mawi- . . . sikuzote kuna matabaka matatu, si *matabaka*, nisingelisema, jamii za watu duniani. Sisi sote tunatoka kwa wana wa Nuhu: Hamu, Shemu, na Yafethi. Sasa, hao walikuwa ni Myahudi, Mmataifa, na Msamaria.

122 Sasa, kwa wahudumu hawa walioketi nyuma yangu hapa, na labda wengine walioketi mbele yangu, sote tunajua ya kwamba Petro alipewa funguo za Ufalme, nipate kunyosha hili kwa ajili yenu kwa neema ya Mungu, Petro alipewa funguo za Ufalme.

123 Sasa, kwenye Siku ya Pentekoste, yeye ndiye aliyewafungulia Wayahudi Ufalme, tunakubali hilo. Na wakati Filipo aliposhuka na kuwahubiria Wasamaria na kuwabatiza katika Jina la Yesu Kristo, ila tu Roho Mtakatifu hakuwa amewashukia bado, na hata hivyo Filipo alikuwa na Roho Mtakatifu, kwa hiyo wakatuma watu wamlete Petro, naye na Yohana wakashuka wakawawekea mikono, nao wakampokea Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli? Vema.

124 Ndipo tunaona ya kwamba alikuwa juu ya dari siku moja, akiona ono, naye Kornelio alikuwa ameona ono, ambaye alikuwa ni Mmataifa, nao wakamtuma nyumbani kwa Kornelio, na huko akawafungulia Mataifa Injili. Hao hapo watu wako watatu: watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Huyu mtume hakutumiwa tena, zile funguo, kuufungua Ufalme, kwa sababu ulikuwa ni kwa ajili ya kila mtu basi.

125 Sasa, tunaona wakati alipokuja, kulikuwako na Mataifa, sisi, Waanglo-Sakson, hatukuwa tukimtazamia Masihi, tulikuwa makafiri, Warumi na kadhalika, tukiabudu sanamu. Lakini kulikuwako na matabaka mawili ya watu, ama jamii mbili, zikimtazamia, hizo zilikuwa ni Myahudi na Msamaria, naye Msamaria alikuwa nusu Myahudi na Mmataifa.

126 Sasa, sikilizeni kwa makini sasa, msije mkalikosa. Sasa, hao, Yeye huja tu kwa wale wanaomtazamia. Hebu nirudie hilo, katika kusanyiko usiku wa leo, kama uko hapa kama mkosoaji, kama uko hapa kama asiyeamini, kamwe hatakugusa, ila kukukemea tu, bali Yeye huja kwa wale wanaomtazamia, ambao ni waaminio. Hakuna mahali popote katika Maandiko alipopata kuja kwa njia nyingine yoyote, ila kwa waaminio, hapo ndipo Yeye aliahidi kukusanyikia. Kufanya uponyaji Wake, Yeye alimwondoa ki—kipofu kutoka kwa wasioamini, akampeleka nje ya mji, ili kuyaponya macho yake.

127 Yeye huja tu kwa waaminio. Kwa hiyo, Mataifa katika siku hiyo hawakuwa wakimtazamia Masihi yeyote, bali Wasamaria na Wayahudi walikuwa wakimtazamia. Naye alipowaja Wayahudi, alionyesha ishara Yake kama Masihi, nao waaminio wa kweli wakatambua kuwa ni Masihi, asiyeamini aliikataa naye akalaaniwa nayo.

128 Sasa—sasa, tunaninii...tunaona basi katika Yohana Mtakatifu mlango wa 4, Yeye anapanda sasa kwenda kule, Samaria, kwenye mji wa Sikari, na wakati anapofika kule juu, anawatuma wanafunzi Wake waende wakanunue chakula. Nao walipokuwa wameenda zao kununua chakula, akatokea mwanamke, mwanamke mwenye sifa mbaya, naye alikuwa... alikuwa na waume wengi, naye akatoka kuja kuteka maji, ndipo Yesu akasema, “Mwanamke, nipe maji ninywe.”

129 Naye akasema, “Kisima ni kirefu, na isitoshe, tuna ubaguzi hapa, kuna...ninyi—ninyi Wayahudi hampaswi kutuomba sisi Wasamaria mambo kama hayo, si kawaida kwa mwanamume wa Kiyahudi kumwomba mwanamke Msamaria.”

Akasema, “Lakini kama ungalijua ni Nani ulikuwa unasema naye,” mnaona, “ungeniomba Mimi maji unywe.”

130 Hayo mazungumzo, Yeye alikuwa akifanya nini? Kuishika roho yake. Hatimaye, Yeye akaona shida yake ilikuwa ni nini, Naye akasema, “Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

¹³¹ Kasema, “Umesema vema. Kwa maana umekuwa na waume watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako. Na katika hilo umesema vema.”

¹³² Mwangalieni mwanamke huyo, hili ni kemeo kwa watu wa siku hizi, mwanamke huyo atasimama katika Hukumu na kuvihukumu vizazi hivi, kahaba huyo mwenye sifa mbaya alisimama na kusema, “Bwana, naona kwamba Wewe ni Nabii. Sisi, tunajua, tunafundishwa ya kwamba Masihi, ambaye anaitwa Kristo, Mtiwa Mafuta, atakapokuja, atafanya ishara hizi. Lakini u Nani Wewe?”

Yesu akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

¹³³ Kusikia hayo, akaacha mtungi wake wa maji akakimbia mjini na kuwaambia, watu wa mji, “Njoni mwone Mtu aliyeniambia yale niliyofanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?”

¹³⁴ Sasa, ndugu na dada wa Canada, hebu na tusiwe watoto, hebu tuiangalie Biblia, kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi jana, kwa Wayahudi na Wasamaria pia, si ingekuwa ni ishara ile ile ya Masihi kwa Mataifa?

¹³⁵ Sasa, baadaye kidogo...Kazi hizo kamwe hazikufanywa mbele ya Mataifa katika siku hizo. Lakini hebu nimalizie nipate kumfikia Mmataifa. Sasa, tunajua ya kwamba tumekuwa na miaka elfu mbili bila kumbukumbu mahali popote ya matukio hayo yote baada ya Pentekoste.

¹³⁶ Tumekuwa na kutokea kuuu kwa makanisa, Martin Luther mashuhuri, John Wesley mashuhuri, nami nimeenda mahali pao na nikasimama kwenye mimbara ya Wesley, ninawazia hilo sasa, iko pembeni, ambapo aliwahubiria watu elfu moja mia tano kila asubuhi, na karibu na kaburi lake, na Mama Susanna, na kote kote sehemu mbalimbali za ulimwengu na watu mashuhuri na kadhalika, lakini enyi marafiki, hatujawahi kamwe, tangu siku za mitume na kule kufa kwa ile huduma ya mwanzoni ya kimitume, hata kufikia ka—katikati ya kanisa...karne ya tatu baada ya kifo cha Kristo, hatujawahi kuwa na huduma hii inayokuja.

¹³⁷ Sasa, Kanisa lilitoka kwenye...Huko kulikuwa ni kule kutoka kwenye Kanisa la kimitume, nalo lilizaliwa kupitia miaka mia kadhaa, yapata miaka mia kumi kule, ama zaidi, ya nyakati tu za giza, ndivyo unavyoitwa. Halafu kwenye, upande *huu* ukatokea katika yale matengenezo ya kwanza, ambayo yalikuwa ni Martin Luther, ndipo akaja John Wesley, halafu ile huduma ya Kipentekoste. Katika wakati huu hapa, tunaishi, ni kule kukusanyika kwa wakati wa kanisa.

¹³⁸ Sasa, angalieni, kama Mungu ni Mungu asiyekosea, kama Yeye ni Yehova Mkuu, hawezi kumtendea mtoto mmoja kwa njia moja, na mwingine, mtoto mwingine, njia nyingine, na yale aliyowatendea, hana budi kututendea sisi, la siyo walipata

kitu ambacho hatukupata. Kwa hiyo kama akiliachilia Kanisa liingie kwa theolojia ya kawaida tu, Yeye alilidanganya Kanisa la Mataifa, halafu, alipoahidi ya kwamba angelipa *zaidi* ya waliyokuwa nayo huko nyuma, kwa hiyo kuna kasoro mahali fulani tusipoipokea.

¹³⁹ Lakini sikiliza, ndugu yangu, dada, usiyaache yapite juu ya kichwa chako, daima hupita juu ya vichwa vya watu, wala hawajui lolote kulihusu. Hawawatambui manabii katika siku zao mpaka walipokufa, wala kamwe hawakumtambua Yesu Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu mpaka alipokufa, akazikwa, na kufufuka tena, hapo ndipo Kanisa lilipoanza kutambua Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu.

¹⁴⁰ Mwangalieni Mtakatifu Patrick na wengi wa watakatifu wa upande huu. Mwangalieni Joan wa Arc, ninyi Wakatoliki hapa, mwangalieni Joan wa Arc. Mlimwita nini? Kanisa lenu lilimchoma kwenye nguzo kama mchawi, kwa sababu aliona maono na kuwaombea wagonjwa, na halafu mkasema alikuwa ni mchawi na mkamchoma moto kwenye nguzo, huku mwanamke huyo akilia apate rehema.

¹⁴¹ Loo, kitu kama zaidi ya miaka mia moja baadaye, mkatambua ya kwamba alikuwa ni mtakatifu. Mifanya nini mpate kutubu? Mliichimbua miili ya hao makasisi waliomchoma moto na kuitupa baharini. Lakini mnaona, alipita moja kwa moja juu ya vichwa vyenu, Mungu alimchukua wala hamkutambua.

¹⁴² Ndivyo ilivyo kwa kila wakati, “Yeye huyaficha kutoka kwa macho ya wenye hekima na akili, na kuyafunua kwa watoto wachanga, walio wanyenyekevu na watakaojifunza.” Kwa hiyo hebu tuamke, ndugu yangu, dada, hebu na tuchukue nukuu la Yesu kwa muda kidogo tu kabla hatujafanyiza mstari wa maombi, Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.”

¹⁴³ Hebu na tuangalie hilo linamaanisha nini, “Siku za Sodoma,” siku za Sodoma kulikuwako na matabaka matatu ya watu: Msodoma; mshiriki wa kanisa vuguvugu, ambaye alikuwa ni Lutu na ulimwengu; na kulikuwa na Ibrahimu, Kanisa teule, lililoitwa litoke, ameketi peke yake mlimani, akishika njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa, akipata mambo madogo ya duniani, bali alikuwa ni mtumishi wa Mungu.

¹⁴⁴ Sasa, Mungu alishuka katika mfano wa Malaika watatu, wawili Wao walishuka Sodoma na kuhubiri na kumwita Lutu kutoka Sodoma kabla ya kuteketezwa kwa Sodoma. Sasa, angalieni jinsi alivyorejea kwenye hilo sasa, kufikia wakati wa kuanguka kwa ule Moto.

¹⁴⁵ Na kama tu—tu—kama tuna akili timamu, tunaweza kuona kwamba mtu katika mafanikio yake ya kuuteka ulimwengu,

amepata kitu ambacho kitauangamiza ulimwengu pamoja na nafsi yake, mabomu ya atomiki na haidrojeni. Na lingeweza kutukia kabla ya mapambazuko, lingeweza kutukia katika dakika chache, ulimwengu mzima huenda ukaingia kwenye hizi spatniki na kusema tu, “Vema, mnataka kuangamia, ama kujisalimisha?” Tungefanya nini? Mnaona?

¹⁴⁶ Nazo ziko mikononi mwa watu wenye dhambi. Vipi kama mtu fulani atakunywa vodka nyingi kupita kiasi siku moja, na kuachilia mojawapo ya makombora hayo? Kila taifa limeyaweza tayari, kuvuta tu. Mbona, ulimwengu usingeweza kuponea hayo.

¹⁴⁷ Na hivyo ndivyo hasa Mungu alivyotabiri ingetukia, “Mbingu na nchi zitawaka moto na kuteketezwa kwa moto mkali.” Kasema, “Kabla haijaja ile siku ya Bwana iliyo kuu na ya kuogofya, ulimwengu utateketezwa kwa moto,” Malaki 4. Kisha kasema, “Wenye haki watatembea juu ya majivu,” majivu ya volkano, “ya waovu,” katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Hiyo ni kweli.

¹⁴⁸ Lakini kabla ya siku hiyo kuja, Yeye alisema, “Nitamtuma Eliya atakayerudisha imani ya watu iwarudie baba-...” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁴⁹ Ilikuwa ni ishara ya nini? Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Sasa, Sara, mke wake, alikuwa mkongwe, Ibra-... alikuwa *Abramu*, siku chache kabla ya hapo, bali jina lake likabadilishwa na Mungu likawa *Ibrahimu*, wakati Mungu alipokuwa amesema naye katika ono.

¹⁵⁰ Lakini wakati yule Malaika alipoketi huku mgongo Wake umeelekezwa kwenye hema, Yeye alisema, “Ibrahimu, yu wapi Sara mkeo?” S-a-r-r-...S-a-r-a, alikuwa S-a-r-a-i, mnajua. Kwa hiyo akasema, “Yu wapi Sara mkeo?”

Kasema, “Yuko hemani nyuma Yako.”

¹⁵¹ Akasema, “Ibrahimu, sitakuficha jambo hili, lakini umenitumainia sasa kwa miaka ishirini na mitano, nami nitakuzuru kwa muhula wa uhai.”

¹⁵² Ninawatakeni ninyi watu, kama kusanyiko lililochanganyikana, ku—kuwa na busara sasa, kuninii, ninapoelezea hili. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] ... akaigeukia hema, akasema, “Mbona Sara amecheka, akisema, ‘*Hivi-na-hivi*. Mambo haya yanawezekanaje?’”

¹⁵³ Sasa, angalieni, angalieni yale Yesu aliyosema, sasa, angalieni ma—maana yake, “Kabla haijaja ile siku ya Bwana...” Katika siku ya kuja kwake Mwana wa Adamu, Mungu atakuwa ndani ya Kanisa akiwafanyia watu ishara ile ile, kwa Kanisa Teule, kama alivyomfanyia Ibrahimu kabla ya kuteketezwa kwa Sodoma, basi angalieni ishara hiyo, ishara ile

ile ambayo Yesu alifanya alipokuwa hapa duniani, iliahidiwa katika siku za mwisho.

¹⁵⁴ Kwa hiyo, “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.” Mngemjuaje? Kulingana na Maandiko, wakati alipojitambulisha Mwenyewe kwa Wayahudi, Yeye alikuwa Nabii aliyejua siri ya moyo wao. Ni wangapi watasema, “Hiyo ni kweli?”

¹⁵⁵ Wakati alipojitambulisha Mwenyewe kwa jamii ya Wasamaria, alijitambulisha Mwenyewe kama Nabii, naye huyo mwanamke akaingia na kuwaambia watu wa mjini, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?” Sasa, hebu nichukue kifungu kinachofuata, nayo Biblia inasema ya kwamba mji mzima, jamii yote kule, walimwamini Yesu, kwa sababu ya yale yule mwanamke aliyosema, juu ya neno la yule mwanamke.

Wazia, Yeye alifanya ishara hiyo wakati mmoja, nayo ikatosha kwa nyakati zote, walisema, “Yeye ni Masihi,” maana Yeye alifanya ishara ya Masihi.

¹⁵⁶ Sasa, kumbukeni, sasa, katika siku hizi za mwisho, angalieni, sio Yesu hapa duniani katika mwili wa kawaida, bali Roho wa Yesu katika mwili wa mwanadamu, ukiwa ni tawi la huo Mzabibu, angefanya jambo lile lile katika mwili wa mwanadamu.

¹⁵⁷ Wakati Kanisa lingekusanyika pamoja, Yeye angejitambulisha Mwenyewe kupitia Kwao, kwa hiyo kama angekuja kwenye kanisa hili usiku wa leo, na kufanya jambo lilo hilo, hivi si tungeweza kuinua mikono yetu na kumshukuru Mungu, kama wale Wayunani walivyofanya? “Tumemwona Yesu.” Hivyo ndivyo alivyokuwa, hivyo ndivyo alivyo, ikiwa Yeye ni yule yule jana, leo na hata milele. Je, hiyo ni kweli? Ni wangapi wangetaka kumwona?

Na tuinamishe vichwa vyetu.

¹⁵⁸ Mungu Mtakatifu na Mwenye neema, huu ni wa—wakati mkuu, huu ni wakati ambapo huenda likamaanisha tofauti kati ya uhai na mauti kwa watu wengi. Huenda ikawa kwenye wakati huu ambapo kungekuwako na mtu ambaye angekuwa mkosoaji ambao huenda wakajitenga na Mungu Milele. Huenda kukuwa na mmoja hapa, Bwana, ambaye amekuwa mkosoaji na angekuwa mwaminio na awe na Uzima wa Milele.

¹⁵⁹ Huenda kukawa na wale, Bwana, hapa walio wagonjwa nao wamekuwa wakienda kanisani na wa—wachungaji waaminifu wamewapaka mafuta na kuwaombea, nao wasingeweza kuishika imani ya kuponywa. Jalia iwe, Bwana, ya kwamba wataona ya kwamba Kristo yeye yule ambaye mchungaji wao amezungumza habari zake, sasa amepandishwa juu kidogo pamoja nasi, ama, karibu kidogo nasi, karibu zaidi, na atajitambulisha Mwenyewe miongoni mwetu, usiku wa leo, ndipo waweze kushika imani wapate kuona, “Naam, Yesu yupo hapa, Yeye yuko katikati

yetu. Ninamwamini Yeye kama Mponyaji wangu, kama Mwokozi wangu.”

¹⁶⁰ Ndipo basi wanaweza kwenda wakishuhudia, wakiufanya ushuhuda wao uvume. Nawe unaweza kuwa Kuhani Mkuu, Nawe ndiye Kuhani Mkuu wa maungamo yao sasa, wakati wanapoweza kweli, kutoka moyoni mwao, kuamini ya kwamba Wewe umeifanya kazi. Tunajua kuhusu kazi yenyewe, tayari imekamilika, bali kujitwalia imani ya kuliadini! “Mambo yote yanawezekana kwao waaminio.”

¹⁶¹ Sasa, Bwana Yesu, afadhali ningekuwa huko ukingoni mwa kijito *kule*, nikipumzika mahali fulani nikivua samaki, ama labda niketi nyumbani kwangu pamoja na mvulana wangu mdogo, hapa leo hii kwenye siku yake ya kuzaliwa, maskini mtoto wangu Joseph, mwenye umri wa miaka sita. Jinsi ningependa kumweka pajani mwangu usiku wa leo, nikiona hayo macho makubwa yakiniangalia na kusema, “Baba,” furaha ambayo Wewe umenipa kwa umri wangu wa makamu. Ningekuwa afadhali *huko* chini ama popote pale kuliko kuwa hapa katika kanisa hili, nikijaribu kuwadanganya watoto wa Mungu.

¹⁶² Mungu, ninaomba ya kwamba kwa namna fulani, ya kwamba kila mmoja hapa ataweza kushika maneno haya machache yaliyokatikatika, Baba. Huenda yalitawanyika, huenda yalinini. . . hayakushindiliwa mioyoni, kama vile nafaka zinavyoshindiliwa kwa kawaida, lakini kama yalitawanyika, jalia yaanguke katika ardhi uliyoiandaa Wewe, na matokeo na sifa zitakuwa ni Zako, Baba, wakati sisi katika kanisa hili, mimi pamoja na kanisa hili, tunapojikabidhi Kwako.

Loo, njoo, Bwana Yesu. Sisi si wengi pamoja usiku wa leo, bali Wewe uliahidi watatu, nasi ni zaidi ya idadi hiyo.

¹⁶³ Na jalia tutakapoondoka hapa usiku wa leo, tukienda katika makazi yetu mbalimbali, jalia tuseme kama wale waliotoka Emau, baada ya ufufuo. Na kwenye asubuhi hiyo kuu ya kwanza, mimea yote ilikuwa imechanua, na Uhai ulikuwa ukichanua, naye akatembea pamoja Naye kando ya barabara, Kleopa na rafiki yake. Ha—hawakutambua Yeye alikuwa ni Nani, lakini basi wakati wa jioni, yapata wakati huu labda, walipokusanyika katika nyumba ya wageni, Yeye alifanya jambo fulani kama tu alivyofanya kabla ya kusulubiwa, nao walijua ya kwamba hakuna mtu mwingine aliyefanya hivyo ila Yeye, ndipo macho yao yakafumbuliwa, nao wakatambua Huyo alikuwa ni Bwana wao, Naye akatoweka machoni pao.

Upesi, wakakimbia kwa wale wanafunzi wengine na kusema, “Kweli, amefufuka.” Baba, ninaomba ya kwamba huo utakuwa ushuhuda wetu usiku wa leo.

¹⁶⁴ Sasa, nilizungumza kuhusu kile ulichokuwa katika siku zilizopita. Nao watu hawa wakainua mikono yao kwamba

walitaka kukuona Wewe. Sasa, iwe hivyo kwetu usiku wa leo, Bwana, kulitimiza Neno Lako, ni kulingana na Neno Lako.

¹⁶⁵ Ulipokuwa hapa duniani, ulisema uliponya, kwa sababu ilikuwa ni kutimiza neno lililonenwa na manabii juu Yako, halafu, Baba, usiku wa leo, Wewe uliahidi mambo haya pia, katika siku hii ya mwisho, kwa hiyo ninaomba ya kwamba utalitimiza Neno Lako usiku wa leo. Tujalie, tunapojikabidhi Kwako. Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba. Amina.

¹⁶⁶ Asanteni kwa wema wenu wa kuningojea kwa muda mrefu sana. Na sasa, sisi, kesho asubuhi, tunakuja mapema kwenye kiamshakinywa.

¹⁶⁷ Halafu basi, sitawaweka muda mrefu sana, lakini tutaita tu, naamini. . . Loo, ngoja, mimi. . . Mlisambaza kadi za maombi? Naam. Vema. Anasema alisambaza kadi za maombi. Ilikuwa ni kitu gani? A ama C? Za C. Vema, sawa. Kutoka moja hadi mia moja? Vema. Hebu tuitishe tu mstari mdogo wa maombi katika dakika moja. Mimi ninaninii tu. . . ninafanya. . . ninajaribu kuona ni njia gani Yeye ataniambia nianzie mle ndani, nianzie wapi. Na kuliacha tu lije niani mwangu na ndipo nitaninii. . . Hatutawaleta wengi kupita kiasi.

¹⁶⁸ Lakini kwa jambo hili tu: Kama—kama Yeye, kama Kristo atakuja miongoni mwetu na kuthibitisha ya kwamba Yeye yupo hapa, ya kwamba Yeye hajafa bali yu hai, si kwamba. . .? Je, hatuwezi kuwa na imani kama ya maskini yule kahaba wa Sikari? Je, hatuwezi kusema sisi wenyewe, kama Wakristo waaminio, “Kweli, Huyu ndiye Masihi, kwa sababu Yeye aliahidi jambo hilo.” *Hili* hapa Neno linalosema hivyo, na Yeye huyu hapa, papa hapa pamoja nasi leo, kutekeleza hilo.

¹⁶⁹ Kwa hiyo, marafiki, ninawatakeni mjue kama ningeweza kuja huko nje na, nasema hili kwa uchaji, si kwa mzaha, bali kwa uchaji, na kuweka ro—robo barabarani, na kuisukuma kwa pua yangu moja kwa moja kwenye barabara kuu hapa, na kushuka kupitia mjini nikiisukuma robo hiyo kwa pua yangu, nikienda kwa mikono na magoti yangu, nipate kuwaona mkiponywa, ningeanza sasa hivi, na kwa tochi, ningeisukuma usiku kucha nione mmeponywa.

¹⁷⁰ Sasa, kweli ninamaanisha hilo, nimekuwa mgonjwa, ninajua ugonjwa ni nini. Lakini hilo halingefaa kitu, tayari umeponywa kwa kupigwa Kwake. Ati mimi nikuwekee mikono? Au wahudumu wakuwekee mikono? Hilo ni sawa, bali hilo si la lazima, jambo pekee unalopaswa kufanya ni kukubali yale ambayo tayari amekufanyia. Unaona?

¹⁷¹ Na sasa, ninii. . . ndugu zetu hapa wamewahubiria vizuri na kwa akili timamu, ya kwamba Yeye ni Kristo, nanyi mkauamini na kuukubali wokovu. Basi mnaona matokeo, jinsi mlivyo na furaha? Vema sasa, jambo lile lile litakuwako kwa ama kwa uponyaji au wokovu, hamna budi kukumbuka, kazi zimekwisha

tayari. Sasa, tutauliza tu kama kila mtu atakuwa na kicho vivyo hivyo.

¹⁷² Sasa, kama Baba yetu Mtakatifu atatumia Uwepo wa Roho Wake, na, kufanya kazi zile zile hapa mbele zenu, ni wangapi hapa ndani hawajawahi kuona hilo likifanywa maishani mwako? Hebu tuone mikono ye—yenu ikiinuliwa. Kote kwenye jengo, hujawahi kuliona maishani mwako mwote. Mnamaanisha kuna watu wawili tu ambao hawa- . . . ?

¹⁷³ Ni wangapi hapa hawajawahi kuwa katika mmoja wa mikutano yangu, inua mkono wako? Kamwe katika mmoja wa mi- . . . Vema, mliona likitendeka wapi basi? Mimi . . . Sasa, kuna kasoro mahali fulani. Hakika, ninaamini ninyi ni waaminifu. Ninyi . . . Vema, labda mlifanya, kwa hiyo ni—ninashukuru kwa hilo.

¹⁷⁴ Lakini, ninaamini ya kwamba kuna kasoro mahali fulani, maana hilo halikutokea sawa, kwa hiyo labda hamkunielewa. Ninaona wakati mwingine hapa ndani, tuna Mnorwe, Mswidi, na kadhalika, ili kwamba wasininii, labda hawafahamu Kiingereza vizuri sana, kwa hiyo labda . . . Lakini mlielewa mara ya pili. Kwa hiyo ni wangapi wanaompenda Bwana? Nitasema hivyo. Sasa, sote tunafanya hivyo. Vema, bwana.

¹⁷⁵ Sasa, hebu tuone. Ulisema C, moja hadi mia moja? Hebu tuanzie namba moja basi. Kadi ya maombi C, namba moja. Umeninii . . . ? Ni nani, aliye na kadi hiyo ya maombi? Je, waweza . . . ? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Inaonekana kana kwamba wote, kila mtu anaweza kutembea, kwa hiyo nitaninii, badala ya kuchukua . . . kushuka kwenda kule kwa kiwete, nitawaleta tu hapa juu.

¹⁷⁶ Sasa, ningetaka kuwaambia jambo moja nyinyi huko nje: Ni wangapi wanaojua ya kwamba Maandiko yanasema ya kwamba Yesu Kristo, sasa hivi, ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Sote tunakubaliana na hilo, naam. Vema.

¹⁷⁷ Sasa, hicho ni Kitabu cha Waebrania. Yeye—Yeye ni Nini? Kuhani Mkuu. Je, Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule aliyekuwa wakati alipokuwa hapa duniani? Yeye ni yeye yule? Basi angetendaje katika ukuhani Wake kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule aliyekuwa jana? Kama yuko leo, angetenda vivyo hivyo, hiyo ni kweli?

¹⁷⁸ Ni wangapi wanakumbuka ile hadithi ya yule mwanamke aliyekuwa anatokwa na damu, aliyekuja akaugusa upindo wa vazi Lake, akisema kama angeweza kugusa vazi Lake angepona? Mnakumbuka hadithi hiyo?

¹⁷⁹ Sasa, sasa, angalieni jambo hili, halafu labda, hebu na tuliseme tu kwa ajili ya ho—hoja fulani, yeye hakuwa na kadi ya maombi, asingeweza kumkaribia, bali akasema, “Ni—ni—

ninaamini kama ningeweza kugusa vazi Lake, nitakuwa mzima.” Kwa hiyo akamyemelea, mpaka akagusa vazi Lake. Kimwili, Yeye asingeweza kulihisi, maana vazi, vazi la Kipalestina, hupwaya pamoja na vazi la ndani.

Kwa hiyo basi yeye... Yeye... Lakini Yeye alisimama, akasema, “Ni nani aliyenigusa?”

¹⁸⁰ Ndipo mtume Petro akamkemea vikali, akisema kitu kama hiki: “Kwa nini useme jambo kama hilo? Kila mtu anakugusa, ‘U hali gani? Wewe ndiwe Nabii? Je, Wewe—Wewe ndiye Mhubiri? Je, Wewe...? Hakika tuna furaha kukutana na Wewe. Tunaninii... Tungependa kuwa Nawe hapa, Kasisi,’ namna hiyo, kila mtu.” Kasema, “Na kusema, ‘Ni nani aliyenigusa?’ Mbona, halisikiki la busara,” huenda Petro alisema.

Kwa hiyo Yesu akasema, “Lakini naona kwamba nguvu zimenitoka.” Hiyo ni kweli? Sasa, nguvu ni uweza, kwa maneno mengine, “Nimekuwa dhaifu.” Mnaona?

¹⁸¹ Sasa, wakati hilo lilipofanyika, Yesu aliangalia juu ya kusanyiko, sikilizeni kwa makini sasa, Yesu aliangalia juu ya kusanyiko Lake, labda kama lililosimama hapa, labda kubwa zaidi, labda si wengi hivyo, bali aliangalia kwenye kusanyiko mpaka akamwona huyo mwanamke, na kumwambia kuhusu kutokwa kwake na damu, na kusema kulikuwa kumekoma, imani yake ilikuwa imemwoko. Hiyo ni kweli?

¹⁸² Vema sasa, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, Kuhani Mkuu yeye yule, na ninyi mnaoketi huko nje hamtakuwa kwenye mstari huu wa maombi, hivi hamngeweza kumgusa Yeye kwa imani yenu? Je, si angetenda vivyo hivyo kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule? Je, hilo linasikika lenye mantiki? Inueni mikono yenu, kila mtu humu jengoni. Mnaona, ninawafanya... kupata kibali cha Mungu nikiweza, kuwafanya mwone kwamba ni kweli, angalieni jinsi mnavoliitikia. Mnaona? Ingekuwa vivyo hivyo.

¹⁸³ Sasa, ninyi huko nje semeni, “Ndugu Branham hajui hata jambo moja kunihusu mimi, yeye ni mgeni kabisa kwangu, hanijui, lakini Bwana, Wewe unajua shida yangu, kwa hiyo kama utamruhusu tu... Ninataka kukugusa Wewe, Yesu. Je, ninaweza kupata—kupata uponyaji wangu usiku wa leo?” Kisha useme, “Nena kupitia Ndugu Branham na hebu ageuke na kuniambia.” Basi angalia kama Yeye anafanya hivyo.

¹⁸⁴ Hilo si lingekuwa zuri sana? Hilo si lingekuwa...? Hilo lingefanya Ukristo vile vile... Mwajua, miungu wengi wakuu wa Buddha, na—na Makalasinga wote, na Wajaini, na kadhalika wa dini mbalimbali, na kila mmoja wa waanzilishi wao wamekufa na wako kaburini, lakini sisi tuna kaburi tupu, Ukristo. Bwana wetu amefufuka katika wafu, Naye yu pamoja nasi, akiishi ndani yetu, akijionyesha Mwenyewe kwa

mathibitisho yasiyoweza kukosea ya kwamba Yeye ndiye Ufufuo na Uzima. Amefufuka katika wafu.

¹⁸⁵ Sasa, yanayofuata itabidi yawe ni Mungu, huu ndio umbali niwezao kwenda, mtu yeyote anajua hilo, yanayofuata hayana budi kuwa ni Mungu. Sasa, msininii. . . Simama tu papo hapo, Mama, ingekuwa sawa sasa.

¹⁸⁶ Sasa, huyu hapa amesimama mama ambaye ni m—mgeni kwangu. Jambo lingine, ningependa kuuliza hivi: Ni wangapi humu ndani ambao ni wageni kwangu, ambao mnajua kwamba sijui lolote kuwahu? Inua mkono wako, unajua kwamba. . . inu- . . katika mstari wa maombi, kila mmoja wenu kwenye mstari wa maombi, kama ninyi nyote ni wageni. Vema, kila mmoja wenu.

¹⁸⁷ Sasa, ha—hatufahamiani mimi na wewe, nina marafiki wawili au watatu hapa, ambao wako hapa likizoni pamoja nami, mhudumu anayeketi *hapa* pembeni, kutoka huko chini A—Alabama, kisha nina Ndugu Sothmann, yeye ni Mkanada, na Ndugu Tom, anayeketi nyuma kwenye kona *hii hapa*, mle ndani, hao *hapo*, papa *hapa* pembeni, kwa hiyo ninawajua.

¹⁸⁸ Sasa, kwa uchaji kabisa na kila mtu katika maombi sasa. Sasa, hii ni picha, kitu kama nilichokuwa nikizungumzia dakika chache zilizopita, cha Yohana Mtakatifu mlango wa 4, Bwana wetu alikutana na mwanamke Msamaria, mwanamke Msamaria kisimani. Je, mnaifahamu hadithi hiyo?

¹⁸⁹ Sasa, Yeye alikuwa ni mwanamume, naye alikuwa ni mwanamke, nao walikuwa wamesimama labda, kama tulivyo sasa, na ki—kisima kwa namna fulani ni mandhari, na—na akaanza kuzungumza naye mpaka akaona shida yake iliku- . . . Aisee, wewe panda hapa juu ukiweza, tafadhali, *hapa* tu, ili lisikuchoshe sana.

Kwa hiyo akazungumza na—na yule mwanamke na kusema. . . Alikuwa akijaribu kuwasiliana na roho yake, bila shaka, wakati aliposema, “Nipe maji ninywe,” Yeye alikuwa akiwasiliana naye.

¹⁹⁰ Sasa, iweni na kicho kabisa, msisogee huku na huku. Mnaona, kila mmoja wenu ni roho, mnajua hilo, kama sivyo, umekufa. Kwa hiyo basi. . . ni roho yako. Na kila moja ya roho zenu sasa anawasiliana na Roho Mtakatifu. Unaona, ni nyeti sana, na Yeye, ni mwepesi sana wa kushtuliwa, ataondoka tu. Mnaona? Kwa hiyo sasa i—i—iweni tu, iweni na kicho na watulivu mwezavyo sasa.

¹⁹¹ Sasa, mnatambua, ninyi Wakristo, kile ninakabiliana nacho? Huyu hapa mwanamke ambaye sijawahi kumwona maishani mwangu. Nami. . . Hatufahamiani. Sasa, ili mpate kujua na kuwa na hakika, angalieni, ninainua mikono yangu, sijawahi kumwona maishani mwangu. Waweza tu kuinua mkono wako

wapate kuona? Inua tu mkono wako kusudi watu waone ya kwamba hatufahamiani.

¹⁹² Sasa, yale nimefundisha usiku wa leo yamekuwa ni Maandiko, yale yaliyokuwa ahadi za Mungu kwa ajili ya siku hii. Sasa, hapa kuna, Ukristo hauna budi kuonyeshwa la sivyo ni wa bandia. Biblia ni ya uongo ama ni ya kweli. Kristo amefufuka au hajafufuka.

¹⁹³ Sasa, haiwezekani kabisa kwangu kumjua mwanamke huyu, chochote kumhusu, kwamba yeye ni nani, anatoka wapi, kilichomleta hapa, shida yake, ama, isingewezekana kabisa kwangu kujua hilo. Ingebidi ifunuliwe na nguvu fulani za kimbinguni. Sisi sote, tungeweza kusema, “Amina,” kwa hilo. Vema, yote ni . . . Inategemea tu kile unachofikiri ilivyo. Unaona? Hiyo ni juu yako. Unaona?

¹⁹⁴ Lakini sasa, kama Yeye angefanya hivyo, na angeniambia jambo fulani lililokuleta hapa, ama kitu fulani ambacho kimekuwako maishani mwako ambacho unajua . . . Sasa, kama nilisema, “Dada, Bwana Yesu aliniita kuwaombea wagonjwa. Unaamini hilo?”

Labda ungesema, “Naam, Bw. Branham, ninaamini hilo.”

Ningesema, “Vema, ni—nitaweka mikono yangu juu yako, na kukuombea.”

Nami ningeweka mikono yangu juu yako, na kusema, “Yesu, Yesu Mpendwa, mponye mwanamke huyu na apate afya.”

¹⁹⁵ Nawe ungesema, “Ninaamini hilo,” uende zako, naamini ungepona. Mimi . . . Mnge—mngeamini hilo, ninyi nyote? Hakika, tungeamini. Mnaona, maana niliuliza. Sasa, hiyo ni kweli, hilo lingekuwa sawa. Lakini sasa, nini . . . ?

Kama tukianza kuzungumza juu ya Kristo aliyefufuka na ahadi ya kujionyesha Mwenyewe miongoni mwetu, mnaona, basi, sasa, hilo linaleta kitu kingine.

¹⁹⁶ Sasa, huyu hapa anakuja hapa na anaweza kukwambia kile umekuwa, ama shida yako, ama kile unachotamani, ama kitu kama hicho, kitu ambacho unajua na unajua kwamba sijui, nawe unajua mimi nikiwa mwanadamu, nisingekuwa na njia ya kukijua, basi hiyo inaonyesha kama Yeye anajua kile umekuwa, Yeye anajua kile utakachokuwa. Hiyo ni kweli, wasikilizaji? Mnaona?

¹⁹⁷ Sasa—sasa, iweni na kicho kabisa. Yeye ni mtu mzuri. Lakini mimi, nimekuja kwenu nimechoka sana, nimekuwa hudumani kwa miezi sita mpaka niko karibu tu kuninii . . . Ndugu Mercier alikutana nami muda mfupi uliopita, kasema, “Ndugu Branham, unaonekana kana kwamba unakaribia tu kuzimia na kuanguka chini.”

Nikasema, “Naam.” Mnaona?

198 Miezi sita ya hii, wakati mwingine maono ishirini na thelathini usiku mmoja, mpaka yananinii—yananiua tu. Basi kumbukeni, mtu mmoja alifanya nguvu zimtoke. Mnafikiri ingenifanyia nini mimi mwenye dhambi, aliyeokolewa kwa neema Yake? Ni kwa sababu tu Yeye alisema, “Zaidi ya hizi mtafanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba.” Maandiko yanapaswa kutimizwa.

Sasa, kama Yeye atanielezea kile—kile kilichokuleta hapa, utajua kama ni kweli ama si kweli. Unaona, wewe. . .

199 Mama huyo anafahamu vizuri sana kuna jambo fulani linaloendelea, ambalo lipo, ninaangalia Nuru inayoshuka moja kwa moja juu yake. Naye mama huyo anaugua wa—wasiwasi mbaya sana hata anataka kuombewa. Hiyo ni kweli. Wasiwasi. Kama. . . Hiyo ni kweli, sivyo?

200 Na halafu uko—uko karibu kufanyiwa upasuaji. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kwa ajili ya uvimbe. Kama Mungu ataniambia huo uvimbe uko wapi, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Uko kwenye pua yako. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

Sasa, unaamini?

201 Sasa, kuna upako hapa mahali fulani. Unatambua ya kwamba jambo fulani linaendelea, hisia tamu kweli, sivyo? Huyo ni Kristo, Roho Mtakatifu. Sasa, inua tu mkono wako kama hiyo ni kweli, unahisi hisia tamu sana. Hii hapa.

202 Sasa, upako huu kwa hili, ninaweka mikono yangu juu ya dada yangu katika Jina la Yesu Kristo, kuzihukumu kazi zote za ibilisi, apate kuponywa. Amina.

Mungu akubariki, Dada. Nenda, na amani ya Mungu iwe pamoja nawe.

Sasa, unaamini ya kwamba Yeye yu hai? Hakika, Yeye yu hai.

203 U hali gani, Mama? Mimi na wewe tukiwa hatufahamiani, hiyo ni kweli. Mara ya kwanza kukutana, lakini Mungu anatujua sote wawili. Kama atanifunulia shida yako ni nini, utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Utaamini.

204 Huko hapa kwa ajili yako mwenyewe, umesimama hapa kwa ajili ya mtu mwingine, rafiki anayeugua kichaa. Hiyo ni kweli, sivyo? Unaamini watapona? Mungu akubariki. Nenda, na amani ya Mungu iwe pamoja nawe, na kile ulichoamini, kitakuwa hivyo tu.

205 Njoo kwenye hili. . .? . . . U hali gani? Je, unaweza kuzungumza Kiingereza? Wewe ni Mhindi? [Dada huyo anasema, “La, Myahudi.”—Mh.] Myahudi. Hilo ni zuri sana. Loo, unapaswa. . . Kuna mema. Sisi hapa. Unazungumza Kiebrania? Kiyidi? Sisi hapa tena, Myahudi amesimama hapa. Basi lingekuwa jambo zuri sana kumwona Masihi.

206 Unajua ukiwa Myahudi, kwamba Masihi alipaswa kuwa yule Nabii ambaye Musa alinena habari zake, angefufuka. Hiyo ni kweli, dada yangu Myahudi? Basi nina hakika hungefanya kosa ambalo makuhani wa hekalu walifanya katika siku za mwanzoni, kulikataa, ungeamini ya kwamba ingekuwa ni Masihi.

207 Hii ni mandhari ya Kibiblia, kwenye wakati huu tu, marafiki, mwanamke wa Kiyahudi, ambaye amefundishwa kuamini ya kwamba Masihi angekuwa ni Nabii. Sasa, hilo. . . Mimi siye Masihi, ni Roho Wake, Roho Mtakatifu, huyo Ndiye. Unaona? Tumetiwa mafuta tu na Roho Wake. Yeye ndiye Mzabibu, mimi ni mojawapo tu ya matawi Yake.

Uko katika hali mbaya sana, unaugua uvimbe. Hiyo ni kweli.

208 Sasa, ninaendelea kuhisi hilo likija kutoka *hapa*, likisema, “Yeye anabahatisha hilo.” Silibahatishi hilo. Sasa, kumbukeni, hamwezi kuyaficha mawazo yenu sasa. Mnaona? Hapa, yeye ni Myahudi. Hebu kidogo.

209 Sijui alisema shida yako ni nini. Mimi. . .Mnaona, ni kama vile ninaenda, ni katika kiwango kingine tu, ulimwengu mwingine. Naam, ni u—uvimbe, na ni uvimbe wa kikoromeo. Hiyo ni kweli, sivyo? Nawe unaugua wasiwasi. Ni kweli. Halafu una ninii, mtu fulani unayemwombea, huyo ni mtoto. Naye ana wasiwasi kupindukia, na IQ ya—yake, ma—masomo si mazuri sana, unaombea hilo. Hiyo ni kweli. Unamwombea dada fulani pia, ambaye anaugua sana, wasiwasi. Bibi Lick, jina lako, unaweza kurudi, umepata haja yako sasa, Jina la Yesu. Unaamini Yeye ni Masihi sasa? Amina. Mungu awabariki.

210 Vipi kukuhusu wewe kwenye kusanyiko? Unaamini kwa moyo wako wote? Yeye ni Kristo, Mwana wa Mungu. Iweni na kicho kabisa. Je, mnatambua ni Nani Mtu huyo aliye miongoni mwetu sasa? “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.”

211 Vema sasa, hutauona mwili Wake wa nyama mpaka Kuja Kwake mara ya Pili. Wala kamwe hatafika duniani katika Kuja Kwake Mara ya Pili, tutanyakuliwa hewani kumlaki hewani. Tutamlaki hewani. Hiyo ni kweli, ndugu? Kumlaki hewani. Lakini Roho Wake. . .

212 Mnaona jinsi Kanisa limekuja kutoka kwa Martin Luther, kuhesabiwa haki, Wesley, kutakaswa, Pentekoste, ni Roho Mtakatifu, kama kule kufunikwa kwa piramidi? Sasa, Yeye anaichonga. Mnakumbuka, kile kichwa cha piramidi nyuma ya dola yetu ya Marekani, Ule Muhuri Mkuu, haukuwepo. Yeye ndiye Jiwe la Kichwa, Lililokataliwa, kwa hiyo analichonga vizuri sana halina budi kutoshea moja kwa moja ndani. Haina budi kuwa ni huduma Yake ikijirudia tena katika Kanisa Lake, kwa ajili ya Unyakuo. Mbona, tuko papa hapa, enyi marafiki.

Unaamini miguu na viganja vyako vitakuwa sawa? Vema, Bwana. Unaweza kuupokea basi. Amina.

213 Mimi ni mgeni kwako, sikujui, lakini Mungu anakujua. Kama Bwana Yesu atanifunulia shida yako ni nini, utaamini ya kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu, nami nimetumwa tu kama mtumishi Wake? Kwa—kwa moyo wako wote.

214 Ni wangapi katika kusanyiko wataamini? Sijawahi kumwona mtu huyu maishani mwangu. Ha—hatufahamiani. Hiyo ni kweli? Inua tu mkono wako, ili kwamba tuone ya kwamba hatufahamiani kabisa.

Sasa, kama Yeye atafanya jambo hili, kama wakati mmoja yule Msamaria aliliona likitendeka naye akashawishika kabisa, hakika tungeweza kushawishika.

215 Mtu huyu amekuwa na matatizo mengi, ametoka hospitalini, ugonjwa wa tezi dume, upasuaji. Unakusudiwa kurudi tena, na hiyo ni kwa sababu ya u—ugonjwa wa bawasiri. Hiyo ni kweli. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.

216 Baba wa Mbinguni, jalia kwamba baraka Zako zikae juu ya maskini ndugu huyu, kwamba ataponywa apate kuishi kwa ajili ya utukufu Wako. Ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu akubariki, Ndugu Mdogo. Nenda, ukiamini sasa, itakwisha kwako. Amina. Mungu awe pamoja nawe, Ndugu.

217 Unaamini sasa kwa moyo wako wote? Ni wangapi wanaoamini sasa kwa mioyo yenu yote? Ni wangapi watakaoukubali sasa kwa moyo wako wote? Mwamini Yeye.

218 Ni sawa, haikukubidi kupanda huku juu kabisa. Vipi kama ningekwambia, bila kukwambia neno moja, ya kwamba shida yako imekwisha, ungeamini? Ungepona? Ugonjwa wa mgongo ungepona, nao ugonjwa wa moyo, kila kitu, ungeendelea tu na uwe mzima? Rudi moja kwa moja, sasa, kitini mwako basi na upokee tu, na uamini kwa moyo wako wote.

219 Sasa, na wewe je? Kama hukupanda vipandio, maskini mama pale, hapa, vipi kama ningekwambia ungeweza kula chakula chako tena, ugonjwa huo wa tumbo umekuacha, ungeamini? Kama ungetaka, inua mkono wako. Basi nenda ukale, Yesu Kristo anakupa afya.

Ugonjwa wa figo, ugonjwa wa mgongo, na kadhalika, tayari umekuacha, unaweza kwenda nyumbani sasa na upate afya. Amini kwa moyo wako wote.

220 Angalia hapa, Bwana. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Unaamini maskini kikohozi hicho cha pumu kitakuacha wala hutakuwa nacho tena? Unaamini? Unaamini kwa moyo wako wote? Basi rudi na uamini, na itakuwa hivyo tu.

Amini tu, usitie shaka. Kama unamwamini Mungu, Mungu atakujalia, kama—kama utaamini.

221 Vipi kama nilikwambia tu ukisimama pale, sikusema jambo moja, nikwambie tu uende kwenye kiti chako, ungekuwa mzima, ungeamini? Nenda kwenye kiti chako na uwe mzima, hivyo tu.

Ninataka tu kuona kile wengine wenu, nione kama mna imani kiasi hicho kuamini.

Ungeamini jambo lile lile? Zidi kusonga mbele, useme, “Bwana abariki.”

²²² Sasa, ungewazia nini kama ningekwambia? Unasema, “Afadhali, Ndugu Branham, ungeniambia kuna shida gani, kwa sababu nina wasiwasi kidogo.” Hiyo si ilikuwa ni kweli? Sisomi mawazo yako, lakini usingeweza kuficha mawazo yako wakati huu. Vema. Shida yako ya kike, shida ya akina mama, itakuacha, kwa hiyo u—unaweza kurudi kwenye kiti chako. Nenda tu naye Ndugu, na uwe mzima. Yesu Kristo, akupe afya.

Mnaamini kwa mioyo yenu yote? Vipi kuhusu huko nje kwenye kusanyiko? Iweni na kicho kabisa.

²²³ Mama huyu aliyeketi hapa nyuma kabisa mwishoni, akiniangalia hapa nje mwishoni, ukiwa na shida na magoti yako, unaamini Mungu atakuponya, Mama? Kwa namna fulani ni mama mnene, sikujui, sijawahi kukuona maishani mwangu, lakini una shida na magoti yako. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

²²⁴ Aligusa nini? Uliza kile alichogusa. Alingusa Kuhani Mkuu, Yesu Kristo, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Unaamini hilo kwa moyo wako wote?

²²⁵ Mama huyu aliyeketi papa hapa, akiugua yabisi kavu. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, Mama? Unaamini kwa moyo wako wote kwamba Yeye atakuponya? Inua mkono wako kama unaamini. Vema. Uligusa nini? Hukunigusa mimi, uko futi ishirini kutoka kwangu, ulingusa Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Amini kwa moyo wako wote nayo itakuacha.

Mtu mwingine humu ndani anaamini?

²²⁶ Hapa, hapa kuna...Wewe uliyeinua mkono wako, unaamini? Unaamini huko nyuma, mama huyo, unaamini kwa moyo wako wote? Ugonjwa wa fadhaa utakuacha. Una ugonjwa wa fadhaa. Hiyo ni kweli. Pia una yabisi kavu, una matatizo. Hiyo ni kweli? Ikiwa hatufahamiani, pungu mkono wako namna *hiyo*. Ulingusa nani? Hukunigusa mimi, ulingusa Kuhani Mkuu. Sasa, ugonjwa wako wa fadhaa umekwisha, unaweza kwenda nyumbani na uwe mzima, katika Jina la Yesu Kristo.

²²⁷ Ni wangapi wenu wanaoamini ya kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, amefufuka katika wafu, na matakwa tunayoomba, “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu,” tunamwona Roho Wake akitenda kazi miongoni mwa watu Wake? Inueni mikono yenu.

²²⁸ Sasa, nitawaomba mfanye jambo fulani. Ni waaminio wangapi waliope hapa? Wote walioinua mikono yao ni

waaminio. Sasa, mwaweza kunifanyia jambo fulani? Weka mikono yako juu ya mtu aliyeketi karibu nawe. Hivi utawawekea tu mkono wako? Angalia kile Yeye amefanya usiku wa leo, angalia tu kile Yeye amefanya. Sasa, ninataka kila mmoja wenu ainamishe kichwa chake. Nitaomba tu dua, ninataka mwirudie nyuma yangu.

²²⁹ Mwenyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uzima wa milele, Mpaji wa vipawa vyote vyema, sasa ninakiri imani yangu Kwako, imani yangu katika Mwanao, Yesu, na katika Maneno Yake yote. Alituagiza twende ulimwenguni kote na kuihubiri Injili, Yeye alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Mimi ni mwaminio, ninamwomba mtu huyu, ambaye nimemwekea mikono yangu, wananiomba. Ninaamini kwa ajili yao, wanaamini kwa ajili yangu, pamoja, tunaamini ya kwamba tumeponywa, kwa sababu tunafuata agizo Lako. Katika Jina la Yesu. Amina.

²³⁰ Sasa, endeleeni kuinamisha vichwa vyenu, weka kichwa chako, jifungie tu pamoja na Mungu. Umeungama. Kristo yeye yule aliyefuka kwenye—kwenye siku ya mwisho, aliyefuka kwenye asubuhi ya Pasaka, yuko papa hapa miongoni mwenu, mtaninii, kumbukeni tu, BWANA ASEMA HIVI, kamwe hamtaona, katika wakati wowote, loo, zaidi, wakati wa kanisa la Mataifa, ishara yoyote itakayofuata hii, iliyo kubwa zaidi. Hii ndiyo ishara ya mwisho kwa Kanisa.

²³¹ Jifungie ndani pamoja na Mungu sasa. Amini. Amini tu ya kwamba Yeye anamimina wema Wake wa Roho Wake mwilini mwako, nawe unaponywa, kwa sababu mwaminio huo ameweka mikono yake juu yako, nawe unahisi baraka Zake.

²³² Sasa, wakati ukiamini kwa moyo wako wote, sasa, nitakuomba, na yeyote yule aliyeweka mkono wako... mikono yao juu yako, anaiwakilisha mikono yangu, mikono yangu inawakilisha mikono ya Mungu. Sasa, kila mmoja wenu aanze tu kuamini sasa kwamba unamwona akija moja kwa moja kwenye kiti chako na kusema, “Mtoto Wangu, yote yamekwisha.”

²³³ Baba yetu wa Mbinguni, katika u—utakatifu wa wakati huu, wakati maamuzi lazima yafanywe ambapo watu wataishi au kufa, hawa Wakristo wamefanya maungamo yao kwa sababu ya Uwepo Wako, na kwamba Maandiko yanatwambia ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho, nao wamewekeana mikono, ambalo ni Neno Lako likiliagiza Kanisa Lako. “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa kamwe.”

²³⁴ Kwa hiyo, Shetani, wewe ni kiumbe kilichoshindwa, kwanza kabisa huna haki ya kisheria kuwatesa watu hawa, wewe ni laghai nasi tunaukabili ulaghai huo. Yesu Kristo alikushinda katika mauti na kufufuka Kwake, Damu Yake ililipa kila

gharama ya dhambi uliyoishawishia familia ya jamii ya binadamu, na sasa, sisi ni wana na binti tena, na Roho Wake aliyetiwa mafuta anazungumza nasi jioni ya leo, kama alivyofanya na Adamu wakati wa jua kupunga, kwa hiyo, huwezi kuwashikilia Wakristo hawa zaidi.

²³⁵ Ninakuapisha, kwa Mungu aliye hai, kwamba uwaache watu hawa wagonjwa, toka ndani yao ili waweze kutoka kwenye jengo hili usiku wa leo bila ugonjwa, kwa imani yenye nguvu sana, itakutoa kwenye mawazo yao na milki zao.

²³⁶ Katika Jina la Yesu Kristo, ninamwagiza Shetani awaache watu hawa, magonjwa haya katika namna ya ugonjwa, ambao ni ibilisi, kuwaacha watu hawa, kupitia Jina la Yesu Kristo.

²³⁷ Huku tumeinamisha vichwa vyetu, ningetaka kuwaulizeni kama kuna mtu aliyepo ambaye hamjui Yesu kama Mwokozi wako na ungetaka kusimama kwa miguu yako na kusema, “Wakati nikiwa Uweponi Mwake, ninataka kuungama dhambi zangu na kusema nimekuwa makosani”?

²³⁸ Huenda ukawa ni mfuasi wa kanisa, bali umekuwa asiyeamini, wala huninii . . . hujaamini mpaka sasa, na sasa unataka kumwamini Yeye, nawe unataka kusimama ku—kushuhudia. Waweza kusimama kwa miguu yako na kusema, “Nitamkubali Yesu kama Mwokozi wangu”?

²³⁹ Je, kunaweza kukawa na mmoja miongoni mwetu ambaye angemwacha huyu Roho mtukufu wa Mwana wa Mungu . . . ? Pia kumbukeni, kabla ya mapambazuko asubuhi, huenda ukawa moja kwa moja katika Uwepo Wake, yeye Yule anayetembea humu jengoni usiku wa leo, kutoa hesabu ya yale utakayofanya na Yeye. Je, mtu huyo yupo hapa ambaye hajawahi kumkubali Kristo na angetaka kumkubali?

²⁴⁰ Je, mtu huyo yupo hapa ambaye amekuwa aliyerudi nyuma na angetaka kumrudia Kristo usiku wa leo, wakati ukiwa katika Uwepo Wake mkuu? Simama kwa miguu yako. Je, kuna mmoja hapa ambaye ni mfuasi wa kanisa wala hajui maana ya kuzaliwa mara ya pili, ku—kuzungumza uso kwa uso na Mungu na kufurahia ushirika wa Roho Mtakatifu, na ange . . . ungetaka kumpokea? Waweza kusimama kwa miguu yako?

²⁴¹ Kama sivyo, basi ni wangapi hapa watakaokubali uponyaji wenu, mtakaosimama kwa miguu yenu? Mungu awabariki. Mungu awabariki. Hiyo ni kweli. Pande zote. Hilo ni zuri sana. Hilo ni sawa. Ukubalini uponyaji wenu. Simameni tu kwa miguu yenu kwa dakika moja, endeleeni tu kusimama. Simameni kwa miguu yenu, kila mtu unayetaka kukubali uponyaji wako.

²⁴² Unaona, Yeye anakuangalia, Yeye anakuangalia moja kwa moja, Yeye yupo hapa. Kumbukeni, ninasema hili katika Jina la Bwana, kwa agizo nililopewa na Malaika aliyetumwa kutoka kwa Mungu.

²⁴³ Kama vile ninyi nyote mmeona, ile Nuru, ambayo Marekani imeipatia hakimiliki huko Washington DC, akitundikwa kwenye Ukumbi wa Kidini wa—wa historia ya kidini, huko Washington DC, ndicho Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichowahi kupigwa picha ulimwenguni kote; imetundikwa kwenye kumbi za Ujerumani ambako wameipigia.

²⁴⁴ ROHO HUYO ASEMA HIVI: Yeye yupo hapa sasa kuponya na kumwokoia kila atakayemwamini Yeye.

²⁴⁵ Kumbukeni. . . Bwana awabariki. Asanteni kwa kusimama. Sasa, wasikilizaji wengine watasimama kwa miguu yenu? Ninyi mlio wazima na mngesimama kwa miguu yenu. Asanteni kwa jioni yenu njema na ushirikiano mzuri. Waweza kuingia kwenye simu kesho mahali fulani huko nje kote mjini, na kuwapigia wagonjwa na wanaoteseka, kusudi Yesu apate kuwaponya wakati tukiwa na mkutano huu mdogo? Mungu awabariki daima.

²⁴⁶ Mnampenda? Inueni tu mikono yenu namna *hii*. Waweza kutupa sauti, Dada? “Nampenda, nampenda.” Ni wangapi wanaoujua wimbo huo? Ni mojawapo wa ninazozipenda sana. Vema. Tafadhali:

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.


Na tuinamishe vichwa vyetu sasa, tunapouvumisha.

Nampenda . . .

Ninawapa mchungaji wenu.

Na . . .

Hata tutakapokutana, kesho asubuhi.

Mungu akubariki, Mchungaji. 

61-0519 Mabwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu
United Church
Dawson Creek, British Columbia Canada

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org